9 JUNI, 2026

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Arobaini na Sita - Tarehe 9 Juni, 2026

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Cecilia D. Paresso) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge karibuni katika Mkutano wetu wa Tatu, Kikao cha Arobaini na Sita.

Katibu.

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Maswali, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, namwita Mheshimiwa *Engineer* Chacha Mwita Wambura Mbunge wa Geita Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 541

Kubuni na Kutekeleza Miradi Mikubwa ya Uzalishaji Mali – Geita Mjini

MHE. KIJA L. NTEMI K.n.y. MHE. CHACHA M. WAMBURA aliuliza:-

Je, lini Serikali itabuni na kutekeleza miradi mikubwa ya uzalishaji mali Geita Mjini ili kuongeza vyanzo mbadala vya mapato?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Chacha Mwita Wambura Mbunge wa Jimbo la Geria Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Manispaa ya Geita inaendelea na utekelezaji wa miradi mikubwa miwili ya uzalishaji mali ambayo baada ya kukamilika kwake itaongeza mapato ya halmashauri. Miradi hiyo ni ujenzi wa jengo la kitega uchumi lenye ghorofa nane unaotekelezwa katika eneo la *GEDECO* katika Kata ya Kalangalala kupitia fedha za mapato ya ndani kwa gharama ya shilingi bilioni 12.9 na ujenzi wa stendi ya mabasi unaotekelezwa katika eneo la Magogo katika Kata ya Bombambili kupitia Mradi wa *TACTIC* kwa gharama ya shilingi bilioni 19.17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango mingine iliyopo ni pamoja na ujenzi wa soko la wafanyabiashara katika eneo la Nyankumbu kwa ajili ya kuboresha mazingira ya kufanyia biashara kwa wajasiliamali na kuongeza mapato ya halmashauri. Tayari shilingi milioni 500 zimetengwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 kupitia mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halmashauri itaendelea kubuni vyanzo vingine vya uzalishaji mali kila mwaka kwa lengo la kuongeza mapato ya halmashauri kwa kuzingatia fursa zilizopo na uwezo wa kibajeti wa kutekeleza miradi itakayoibuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Engineer* Kija Ntemi, maswali ya nyongeza.

MHE. KIJA L. NTEMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Tunashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona sehemu nyingi sana za nchi yetu Tanzania yakijengwa masoko ya wajasiriamali almaarufu Wamachinga; je, lini Serikali itakuwa na mpango wa kuwajengea wananchi wa Geita soko la wajasiriamali almaarufu Wamachinga ili kuweza kuwapatia na kuwaongezea mapato katika Jiji na Mji wa Geita? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali ambao umeendelea kutekelezwa ni kuhakikisha inatengeneza na kuboresha mazingira bora ya wafanyabiashara wadogo wadogo, lakini pia wafanyabiashara maarufu kwa jina la Machinga na ndiyo maana katika kipindi cha miaka mitano Serikali imejenga masoko makubwa ya Machinga katika mikoa mbalimbali ikiwemo hata hapa Jiji la Dodoma tuna jengo kubwa na zuri kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo *Machinga Complex*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Katoro, *Engineer* Ntemi kwamba mpango huu wa Serikali ni endelevu na ndiyo maana katika Jimbo la Geita Mjini tayari tumeanza ujenzi wa soko tuko takribani 22% na mpango wa Serikali ni kwamba soko hili likamilike ndani ya mwaka ujao wa fedha ili kutengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya wananchi na wafanyabiashara wadogo wadogo na Machinga kunufaika na shughuli hizo zafanyabiashara.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jafari Chege, swali la nyongeza.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya miradi mikubwa ya uzalishaji ambayo na sisi kama Wilaya ya Rorya tungetamani kupata ni pamoja na soko kubwa la samaki pale kwenye Mamlaka ya Mji Mdogo Shirati. Je, lini Serikali itatupa fedha kwa ajili ya ujenzi wa soko hili?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Wambura Chege, Mbunge wa Jimbo la Rorya amefuatilia mara kadhaa kuhusiana na ujenzi wa soko la samaki katika Jimbo la Rorya na mimi nimhakishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunafahamu biashara na shughuli za kiuchumi za masuala ya uvuvi katika Jimbo la Rorya ni shughuli za kimsingi na ndiyo maana Serikali imeendelea kupitia miradi ya kimkakati ambayo inaandaliwa na halmashauri ikiwemo Halmashauri ya Rorya kuhakikisha tunatenga fedha kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa masoko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishieMheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itaendelea kutenga fedha kuhakikisha soko la samaki katika Jimbo la Rorya linajengwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Charles Mahera, swali la nyongeza.

MHE. DKT. WILSON C. MAHERA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Wilaya ya Butiama ni miongoni mwa wilaya ambazo mapato yake yako chini sana, lakini pia wananchi wa eneo la Kiabakari ambayo ni eneo linaibukia kwa kukua kwa kasi kubwa hasa akinamama wanafanya biashara pale, lakini hakuna soko na eneo hilo Wilaya ya Butiama imetenga eneo la kujenga soko katika eneo la Kiabakari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa je, ni lini Serikali itaisaidia Halmashauri ya Wilaya ya Butiama nayo iweze kuwa na soko kubwa ili iweze kuongeza kiwango chake cha mapato?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nakubaliana na Mheshimiwa Dkt. Wilson Charles Mahera, Mbunge wa Jimbo la Butiama kwamba Halmashauri ya Butiama ni moja ya halmashauri zenye mapato madogo sana ya ndani na moja ya mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba tunapunguza utegemezi wa halmashauri kwa fedha za Serikali Kuu na tunapunguza kwa kuongeza vyanzo wa mapato ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nitumie nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kuhamasisha wananchi, lakini na Halmashauri ya Butiama kutenga eneo maalum kwa ajili ya kujenga soko ambalo kwanza itakuwa ni huduma kwa wananchi, lakini pili itaongeza mapato ya ndani ya halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu kwamba Serikali Kuu tutaunga mkono juhudi za halmashauri, lakini kwa sasa halmashauri waanze kutenga angalau fedha kidogo kwa ajili ya kuanza ujenzi wa soko katika eneo la Kiabakari ili baada ya hapo Serikali kwa kadri ya bajeti tuendelee kuunga mkono na kuhakikisha kwamba soko linajengwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Issa Mchungahela, swali la nyongeza.

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inao mpango maalum, hali kadhalika mradi wa kuendeleza miji kwa maana ya *TACTIC,* lakini je, Serikali ina mpango gani au ina mradi gani kwa kuendeleza vijiji vinavyoibuka na kuwa kama miji ambavyo siyo rasmi mpaka

sasa hivi bado kama vile Mbuyuni, Nachungutwa na maeneo mengine?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuweka mipango inayogusa shughuli za maendeleo na miradi ya kimkakati katika halmashauri mbalimbali kote nchini zikiwemo halmashauri za majiji, manispaa, miji pamoja na halmashauri za wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu Mbunge wa Jimbo la Lulindi, Mheshimiwa Mchungahela anafahamu kwamba katika Halmashauri ya Masasi Vijijini tumeendelea kupeleka fedha kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu na ninafahamu ipo miji ambayo inaibukia kama Mbuyuni, Nachungutwa na maeneo mengine nimhakishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu kama barabara, masoko na *stand* kwa miji yote ambayo inaibuka kwa kadri ambavyo fedha zinaendelea kutafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika miji hiyo kwa kadri inavyoendelea kukua tutaendelea kutenga fedha ili kuendelea kuboresha miji hiyo iweze kufanana na hadhi za miji.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yohana Msita, swali la nyongeza.

MHE. YOHANA S. MSITA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, kwa kuwa Mji wa Itigi ni miongoni mwa miji inayokua kwa kasi na kwa haraka na kwa sababu hiyo mpaka sasa tunavyozungumza mji ule hauna soko kubwa, zuri na la kisasi na Mheshimiwa Naibu Waziri alishafika.

Sasa je, Serikali ina mpango gani wa kutujengea soko kubwa, zuri na la kisasa kwenye mji wetu wa Itigi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri wiki moja iliyopita nilishiriki katika ziara ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Jimbo la Itigi na ni kweli kama ambavyo amesema Mheshimiwa Mbunge Msita kwamba Jimbo la Itigi na Halmashauri ya Itigi ni moja ya halmashauri ambazo zinakuwa kwa kasi sana.

Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tumeshaweka mpango kwanza tulikubaliana siku ya ziara Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba tumetenga eneo kubwa kwa ajili ya kujenga stendi lakini tunaendelea kutafuta eneo kwa ajili ya kujenga soko kubwa litakaloendana na Mji wa Itigi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mpango huo utaendelea kutekelezwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Haidary Sumry, swali la nyongeza.

MHE. HAIDARY H. SUMRY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, katika Manispaa ya Mpanda kuna uendelezaji wa masoko mawili ambayo yako kwenye kata; Soko la Samaki Makanyagio na Soko la Matunda Kawaenzi. Masoko haya yanajengwa kupitia mapato ya ndani na kupelekea sasa kujengwa taratibu kidogo kidogo kulingana na na uhaba wa pesa kutokana na mapato ya halmashauri.

Sasa ni lini Serikali itaunganisha nguvu na Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda ili kuyamaliza haya masoko ambayo ni muhimu sana kwa wananchi wa Mpanda Mjini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda ni moja ya mashauri ambazo zinakuwa kwa kasi na ndiyo maana kwanza Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuboresha miundombinu ya

Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda tumeanza kutekeleza Mradi wa *TACTIC* na nafahamu Mradi wa *TACTIC* tutaboresha barabara na miundombinu mingine katika Manispaa ya Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, lakini Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda kwa kuanza kutenga fedha za mapato ya ndani na kuendelea na uboreshaji wa masoko hayo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tuendelee, safari ni hatua baada ya ukamilishaji wa miradi ambayo ipo kwenye mpango wa *TACTIC* tutaendelea kuona namna nzuri ya kuunga mkono juhudi za halmashauri katika kuboresha masoko haya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Isack Copriano.

MHE. ISACK J. COPRIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anajua fika Mji wa Mto wa Mbu ni mji ambao ni wa kitalii na ni mji ambao kimsingi ndizi nyingi zinapatikana na kumekuwa na ahadi nyingi ya viongozi wanaposimama Mto wa Mbu juu ya lile soko.

Je, ni lini sasa Serikali itatimiza ahadi hiyo ya kujenga soko hilo Mto wa Mbu ili kuondoa uuzaji wa ndizi barabarani?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Monduli Mheshimiwa Copriano Kadogoo Isack amefuatilia mara kadhaa kuhusiana na ujenzi wa soko katika eneo la Mto wa Mbu. Tunafahamu Mji wa Mto wa Mbu unakuwa kwa kasi, lakini ni mji wa kitalii na tutaendelea kuhakikisha kwamba tunatenga fedha kwenye bajeti zetu kwa ajili ya kuanza ujenzi wa soko la kisasa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kumwelekeza mkurugenzi kuanza angalau na mapato ya ndani kwa ajili ya hatua za awali za ujenzi na baadaye Serikali itaona namna nzuri ya kuendelea kushirikiana nao kukamilisha ujenzi wa soko hilo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya kwamba Serikali ina mpango wa kuleta Mradi wa *TACTIC* katika Mji wa Bunda, tunashukuru kwa sababu mmetuhakikishia *tier three* itajengwa, lakini pia lipo soko la kimkakati la Manjebe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja Bunda mazingira yake siyo mazuri na kusababisha wafanyabiashara wengi kutokwenda. Nini sasa Serikali inawaahidi nini Wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini kulitengeneza Soko la Manjebe ili wafanyabiashara waweze kufanya biashara katika mazingira yaliyo bora?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, katika halmashauri zetu yako masoko ambayo pamoja na kutoa huduma za kijamii na kiuchumi, lakini ni chanzo cha mapato kwa halmashauri. Ninafahamu kwamba kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge Ester Bulaya kwamba wanao mpango mzuri wa awamu ya tatu wa *TACTIC* ambao utaboresha miundombinu mingi ambayo ni fedha kutoka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuwasisitiza wakurugenzi wote kote nchini akiwemo Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda kwamba masoko yetu ambayo ni vyanzo vya mapato na tunakusanya ushuru katika maeneo hayo ni muhimu kuhakikisha fedha za mapato ya ndani angalau

zinaboresha miundombinu muhimu kama vyoo, maji, usafi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge natumia nafasi hii kumwelekeza mkurugenzi haraka iwezekanavyo wafike wafanye tathmini ya miundombinu muhimu, waweze kuboresha kwa bajeti ya dharura kupitia mapato ya ndani wakati Serikali kuu inaendelea na taratibu nyingine kwa ajili ya kulijenga na kuliboresha zaidi soko hilo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Thomas Maganga, swali la nyongeza.

MHE. THOMAS K. MAGANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kutupa fedha nyingi za kujenga soko la kisasa pale Halmashauri ya Wilaya ya Mlele eneo la Kalovya limejengwa soko zuri sana, kubwa na la kisasa, changamoto iliyoko pale ni njia za kuingia na kutoka ambazo kwa kweli sio nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kutenga fedha ili tupate njia za lami za kuingia na kutoka kwenye soko lile ili ziendeleze ubora wa soko lile?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, masoko yetu ni vyanzo vya mapato, lakini sehemu muhimu sana za huduma na moja ya vipaumbele vya miundombinu katika masoko ni kuhakikisha kwamba yanaingilika kirahisi, lakini pia kunakuwa na barabara nzuri za kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii nimsisitize Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mlele, lakini na Meneja wa *TARURA* Wilaya ya Mlele kufika katika soko hilo na kuona

gharama zinazohitajika kwa ajili ya kuboresha barabara za kuingia na kutoka kwenye soko hilo ili tuweze kutenga bajeti kwa ajili ya kujenga barabara na kuboresha mazingira ya soko.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Agnesta Kaiza, swali la nyongeza.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jinsi ambavyo umekuwa ukijibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge yanohusu changamoto za wananchi wetu kwa ufasaha mkubwa sana na kupongeza. Nina swali dogo la nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Kipawa ndani ya Jimbo la Segerea ni kata yenye wakazi zaidi ya 77,000 haina soko kabisa, ningeomba kufahamu na kwa kuwa Jiji letu la Dar es Salaam kwa maana ya Halmashauri ya Ilala tuko vizuri chini ya Mkurugenzi wetu kimapato hatuna shida kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kufahamu kauli ya Serikali kuhusiana na wananchi wa Kata ya Kipawa 77,000 ambao hawana sehemu kabisa ya kupata huduma zao za kila siku?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Segerea, amekuwa mfuatiliaji sana wa maslahi ya wananchi wa jimbo lake na mimi nikuhakikishie Ofisi Waziri Mkuu, TAMISEMI tutaendelea kukupa ushirikiano kesho kwamba Wananchi wa Jimbo la Segerea wananufaika na matunda ya Serikali yao usikivu ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu na kwa kweli narejea kumpongeza Mkurugenzi wa Halmashauriya Jiji la Dar es Salaam ndugu Elihuruma pamoja na Mkurugenzi wa Temeke na Wakurugenzi wote kote nchini. Nikimkumbuka pia Mkurugenzi wa Jimbo langu la Wanging'ombe ambaye ameonesha mfano wa kutenga fedha nyingi za mapato ya ndani kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya wananchi katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na kasumba ya baadhi ya wakurugenzi kutotenga fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya kuboresha miundombinu wakisubiri fedha za Serikali Kuu. Maelekezo ya Serikali ni kwamba lazima fedha za mapato ya ndani zitatue kero na changamoto za wananchi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi pia kumsisitiza Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, najua wana uwezo na dhamira wanayo na uwezo wanao wafike katika eneo la Kata ya Kipawa, waainishe eneo kama halipo ili tuweze kukubaliana kuanza kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa soko katika kata hiyo yenye wananchi wengi huduma hiyo ni muhimu sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, katika Manispaa ya Shinyanga kuna soko kuu la mkoa ambalo linajengwa takribani miaka mitano sasa, wafanyabiashara walipisha ujenzi ule, lakini imekuwa ni muda mrefu halijakamilika. Je, ni lini soko lile litakamilika kujengwa?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava kwa wafuatiliaji, lakini ninaomba nimwahidi kwamba mara baada ya kumaliza kujibu maswali hapa mimi na yeye tutawasiliana na Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga ili tuweze kuona nini

kimekwamisha ukamilishaji wa soko hilo kwa muda mrefu, kwa sababu kwa kufanya hivyo tunaathiri ustawi wa wananchi na hivi tuweze kutumia nafasi hiyo kusukuma ili mkandarasi aweze kukamilisha ujenzi wa soko hilo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Boniphace Getere, swali la nyongeza.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia masoko na minada, baadhi ya vijiji na maeneo mbalimbali ya kata yameanzisha minada na masoko, lakini vyanzo vya mapato vya vijiji hivyo na minada kwenye maeneo mbalimbali havirudishi kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sera ya Serikali ya halmashauri ziko wazi. Kwa nini sasa mapato ya 20% ya vijiji hayarudishwi?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali imekwishaweka sheria na kanuni za kurejesha sehemu ya mapato ya ndani yanayokusanywa katika vijiji ili yaweze kurudishwa katika vijiji husika kwa shughuli za uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii niwasisitize Wakurugenzi wote wa Mamlaka Serikali za Mitaa kote nchini kuzingatia utekelezaji wa sheria hiyo. Kwamba baada ya kukusanya mapato kwenye vijiji na kata wahakikishe ile asilimia ambayo wanatakiwa kurejesha kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za kata na kijiji husika zirejeshwe na sisi tuweze kufuatilia kuona namna ambavyo halmashauri zinazingatia maelekezo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Getere tutafuatilia na tutaona hatua za kuchukua kwa halmashauri ambazo hazizingatii sheria ambayo tayari inawaelekeza kufanya hivyo.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea. Sasa ninamwita Mheshimiwa Juma Mustafa Kawamba, Mbunge wa Igalula, aulize swali lake.

Na. 542

Ujenzi wa Daraja Kijiji cha Vumilia na Itulu-Katavi

MHE. JUMA M. KAWAMBA aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga daraja kati ya Kijiji cha Vumilia na Itulu kutokana na changamoto ya kujaa kwa Mto Wara wakati wa masika?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Mustafa Kawamba, Mbunge wa Jimbo la Igalula kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua changamoto inayowakabili wananchi wa Kijiji cha Vumilia, Wilaya ya Uyui na Itulu katika Manispaa ya Tabora hususan wakati wa masika ambapo kukosekana kwa daraja husababisha kukatika kwa mawasiliano na kuathiri shughuli za kiuchumi, kijamii na upatikanaji wa huduma za msingi ikiwemo afya na elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali imetenga shilingi milioni 10 ikiwa bajeti kwa ajili ya kufanya

usanifu wa ujenzi wa daraja hilo kwa lengo la kubaini gharama halisi za ujenzi wa daraja husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya kujua gharama halisi za kutekeleza ujenzi daraja hilo, Serikali itatafuta fedha za ujenzi wake ili kuondoa changamoto inayowakabili wananchi wa Vijiji vya Vumilia na Itulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuzihudumia barabara za Jimbo la Igalula kwa kuzijenga, kuzikarabati na kuzifanyia matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Juma Mustafa Kawamba, maswali ya nyongeza.

MHE. JUMA M. KAWAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza kabisa ninaipongeza Serikali kwa kazi nzuri inazoendelea kufanya kwenye sekta ya barabara nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la nyongeza; Serikali haioni haja ya kutenga fedha kwa ajili ya kutatua vikwazo vya madaraja yaliyomo ndani ya Igalula katika kata zifuatazo; Kata ya Tura, Daraja la Tulieni Mihama katika Kijiji cha Karangasi; Kata ya Kizengi, Daraja la Mdaki, lakini Kata ya Mmale, Daraja la Mbulumbulu katika Kijiji cha Mbulumbulu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali haioni haja ya kujenga barabara kutoka katika Kijiji cha Kawekapina, Idete, Vumilia kwenyewe hadi Kijiji cha Ipululu ili kuweza kurahisisha shughuli za kilimo na kiuchumi ambazo zinaendelea katika Kata hii ya Igalula kwa ajili ya kuchochea maendeleo kwa wananchi wa Kata ya Igalula? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa

Mwenyekiti, ahsante sana, Mbunge wa Jimbo la Igalula kaka yangu Mheshimiwa Juma Mustafa Kawamba amefuatilia mara kadhaa kuhusiana na uboreshaji wa miundombinu ya barabara, madaraja na makalvati katika Jimbo la Igalula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie kama ambavyo katika miaka yote iliyopita ya fedha Serikali kila mwaka imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha barabara, madaraja na makalvati katika Jimbo la Igalula na katika mwaka ujao wa fedha tunakwenda kujenga Daraja la Vumilia kwa kufanya kwanza usanifu, kujua gharama na baadaye Serikali itafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na madaraja mengine ambayo Mheshimiwa Mbunge umeyataja, nikuhakikishie kwamba Serikali inaona umuhimu wa kuendelea kutenga fedha kwa awamu ili kuhakikisha kwamba madaraja hayo yote yanajengwa na kuboresha shughuli za usafiri kwa wananchi wa Jimbo la Igalula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili kuhusiana na barabara Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie bajeti ya Jimbo la Igalula *TARURA* imeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka na dhamira ya Serikali ni kuendelea kuongeza bajeti kuhakikisha kwamba tunaboresha barabara hizo ili kusaidia kuboresha shughuli za kiuchumi kwa wananchi wa Jimbo la Igalula.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, swali la nyongeza.

MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani wa kulijenga Daraja la Videte ili kuliunganisha Jimbo la Mkuranga na Jimbo la Chamazi kwa ajili ya kuondoa msongamano katika Barabara ya Kilwa?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa

Mwenyekiti, tunavyo vipaumbele vingi vya ujenzi wa madaraja katika halmashauri mbalimbali ikiwemo katika Jimbo la Chamazi kwa Mheshimiwa Chaurembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba daraja hilo ni muhimu kwa sababu litapunguza foleni katika Barabara ya Kilwa, lakini ni muhimu pia kwa shughuli za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa sababu tuna miradi ya *TACTIC*, tuna miradi ya *DMDP II,* lakini na miradi ya fedha za mapato ya ndani pamoja na miradi ya *TARURA* bajeti kila mwaka, tutaendelea kutoa kipaumbele katika eneo hilo ili tuweze kujenga daraja na kuhakikisha kwamba tunaboresha usafiri katika maeneo hayo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi ya swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumapili juzi nilikuwa jimboni, Kata ya Sanje ambako wananchi waliniita kwa ajili ya dharura ya Kivuko cha Kisewe ambacho kimekatika na nimeongea na viongozi wa *TARURA* tuone namna gani ya kufanya pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kauli ya Serikali kuokoa wananchi wale ambao wanateseka sana pale Kata ya Sanje kwa ajili ya kivuko, daraja dogo la Kisewe kwenda Kilurumbu?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nitumie nafasi hii kutoa kauli ya Serikali kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amehitaji kwamba maeneo yote ambayo ni barabara kuu na tegemeo kubwa la wananchi wetu katika halmashauri zetu kote nchini, ni kipaumbele kwa mameneja wetu wa *TARURA* wa mikoa na

wilaya pale zinapokatika kufika mapema iwezekanavyo na kufanya tathmini na kujua gharama za fedha zinazohitajika na kufanya matengenezo ya dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Serikali imekwishatoa maelekezo kwanza kutangaza zabuni zote 60% ya bajeti kwa ajili ya kwenda kurekebisha maeneo ya barabara za dharura ambazo ni muhimu.

Kwa hiyo, nitume nafasi nimwelekeze Meneja wa *TARURA* wa Wilaya ya Kilombero pamoja na Mkoa wa Morogoro wafike katika eneo hilo la daraja lililokatika kutokana na muhimu wao wafanye tathmini kwa haraka tuweze kujua gharama zinazohitajika ili Serikali iweze kufanya matengenezo na kurejesha shughuli za usafiri kwa wananchi wa eneo hilo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa ujenzi wa Daraja la Gamaloha linalounganisha kata mbili; Munza na Migato upo kwenye mpango muda mrefu. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za ujenzi wa daraja hilo? Daraja hilo ni muhimu sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa madaraja una hatua kadhaa. Hatua za kwanza huwa ni kufanya usanifu na tathmini ya gharama zinazohitajika na hatua hiyo mara nyingine huchukua muda kidogo na baadaye Serikali huandaa taratibu za kibajeti kwa ajili ya ujenzi wa madaraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwanza Serikali inatambua juu ya

umuhimu wa daraja hilo, lakini Serikali inaendelea na taratibu za kibajeti na mara ambapo tutakuwa tumekamilisha taratibu za kibajeti tutahakikisha tunatoa kipaumbele kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daraja hilo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Suma Fyandomo, swali la nyongeza.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kunipa swali dogo la nyongeza na ninaishukuru sana Serikali kwa kutupatia fedha ya kujenga Daraja la Mafurasopo lililopo Tukuyu Mjini, Wilaya ya Rungwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, daraja hilo ni la muhimu sana linaunganisha kata tatu; Kata ya Ibigi, Buriaga na Bagamoyo, lakini mpaka sasa hivi halijaanza kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wanawake wanasumbuka sana namna ya kuvuka pale pamoja na wananchi wote kwa ujumla; sasa je, ni lini Serikali itaanza ujenzi kwa haraka wa daraja hilo? Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii nimpongeze dada yangu Mheshimiwa Suma Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Mbeya kwa ufuatiliaji wake wa karibu sana kuhusiana na ustawi wa wananchi wa Mkoa wa Mbeya na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu kwamba tunafahamu kuna uhitaji mkubwa sana ujenzi wa madaraja, pamoja na daraja hilo lakini yako madaraja mengine katika Wilaya ya Rungwe ambayo nahitaji ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumwelekeza Meneja wa *TARURA* Wilaya ya Rungwe ikiwa bado hatujafanya tathmini na kujua gharama za ujenzi na usanifu wa daraja hilo

ufanyike mpango kwa haraka, ifanyike tathmini na usanifu ili tuweze kujua gharama inayohitajika kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo na Serikali iweke mpango sasa kwa ajili ya kuanza taratibu za ujenzi wa daraja.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea. Sasa ninamwita Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Tabora Mjini aweze kuuliza swali lake.

Na. 543

Ujenzi wa Barabara ya Kutoka Kata ya Tumbi-Kipera-Itema

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Tumbi - Kipera - Itema ili kuondoa changamoto ya usafiri kwa wananchi wa Kata ya Tumbi?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Jimbo la Tabora Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikikarabati barabara ya kutoka Kata ya Tumbi – Kipera - Itema yenye urefu wa kilometa 9.78 kwa kiwango cha udongo kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 matengenezo ya kuinua tuta kilometa moja, Kujenga makalavati mistari mitatu na kuweka changarawe mita 500 yanaendelea katika Barabara ya Tumbi – Kipera - Itema ambapo shilingi milioni 29.9 zinatarajiwa kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa tayari mkandarasi amekwisha kamilisha ujenzi wa mistari mitatu ya makalvati, uinuaji wa tuta unatarajiwa kuanza mara baada ya maji yaliyokuwa yametuama eneo hilo la mradi kukauka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali imetenga shilingi milioni 70.6 kwa ajili ya kuendelea na matengenezo ya Barabara ya Tumbi – Kipera - Itema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuuhudumia mtandao wa barabara wa Wilaya ya Tabora ikiwemo Barabara ya Tumbi, Kipera na Itema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, maswali ya nyongeza.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ningependa kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuidhinisha zaidi ya shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa barabara katika Jimbo la Tabora Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru sana Serikali, lakini pamoja na fedha hizo ningeomba sana Mheshimiwa Waziri mimi baada ya Bunge tuongozane ili uende ukaangalie kero na changamoto ya barabara katika Jimbo la Tabora Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili linahusiana na barabara zilizopo katika Kata ya Cheyo. Hii ni Barabara ya Masubi - Cheyo B hadi Makutano ya Kilimatinde; Barabara ya *Mwanga Shop* inayoanzia kwa Mrema mpaka *Mwanga Shop* - Mnarani na Barabara ya Mayeye inayoanzia Zebra mpaka *Georgies Complex* kupitia *TDFT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hizi zimekuwa ni changamoto kubwa sana kwa wakazi wa Kata ya Cheyo, Jimbo la Tabora Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kauli ya Serikali juu ya kwenda kuwanusuru na mashimo ya barabara hizi katika Kata ya Cheyo?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimpongeze sana Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Tabora Mjini, amekuwa mfuatiliaji wa mara kwa mara wa ustawi wa wananchi wa Jimbo la Tabora Mjini na kwa kweli ni Mheshimiwa Mbunge ni mchapakazi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali sikivu ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan dhamira yake ni kuhakikisha kwamba tunatua kero mbalimbali zikiwemo kero za barabara katika Jimbo la Manispaa ya Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipokee pongezi na shukrani nyingi ambazo umempa Mheshimiwa Rais na kwa hakika Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana katika uboreshaji wa miundombinu ya barabara kote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa katika Manispaa ya Tabora mnao Mradi wa *TACTIC* ambao nao utajenga barabara za lami lakini utajenga miundombinu mingine, pamoja na mradi wa *TACTIC* tuna mradi wa *TARURA* ambao unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie kwanza niko tayari kuongozana naye baada ya kumaliza Bunge tutapanga kufika katika eneo hilo kwa ajili ya kukagua barabara, lakini kubwa kuhakikisha kwamba tunasukuma utekelezaji wa barabara hizo ili wananchi wapite kwa ufanisi mkubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili kuhusiana na kata hiyo ambayo umeitaja Kata ya Cheyo ambayo ina changamoto kubwa ya barabara. Nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI nimwelekeze Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Tabora na Meneja wa *TARURA* wa Wilaya ya Tabora kufika katika barabara hizo ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja kufanya tathmini, kujiridhisha kama ziko kwenye 60% ambayo tunaendelea na kutangaza zabuni sasa, basi wakamilishe zabuni mapema iwezekanavyo ili wakandarasi waende *site* kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo na ikiwa hazipo kwenye 60% tuweze kuona utaratibu wa dharura kwa ajili ya kurekebisha maeneo ambayo yamekwamisha kupitika kwa barabara hizo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zacharia Paulo, swali la nyongeza.

Waheshimiwa Wabunge, mliowasha *microphones* ninaomba wote mzime.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa barabara nyingi za Jimbo la Mbulu Mjini na baadhi ya maeneo hapa nchini hazijaweza kutengenezwa kwa msimu huu na kwa kuwa mwezi wa 10 pengine mvua za masika zitaanza kunyesha.

Je, ni lini Serikali itaanza kutengeneza barabara hizi zote ambazo bado hazijatengenezwa katika mwaka wa bajeti wa 2025/2026?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimhakikishie Mheshimiwa Zacharia Issaay, Mbunge wa Jimbo la Mbulu na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba hivi sasa tayari Serikali imekwishatoa kibali cha kutangaza zabuni za barabara 60% ya bajeti ya kila halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hivi sasa tayari tuko hatua za mwisho za kuwapata wakandarasi, maana yake kuanzia mwezi huu wa sita mwishoni na Julai, Agosti, Septemba barabara nyingi ambazo zimeathirika na mvua za msimu uliopita zitakuwa zimetengenezwa na zitakuwa zinapitika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge hatutasubiri mpaka msimu mwingine wa mvua kwa sababu tayari Serikali imeshachukua hatua na barabara hizo tuhakikisha pia barabara za Mbulu Mjini nazo zinafanyiwa matengenezo.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea. Sasa ninamwita Mheshimiwa *Engineer* Fadhili Sandali Chilombe, Mbunge wa Tunduru Kusini aweze kuuliza swali lake.

Na. 544

Udhibiti wa Makorongo katika Vijiji vya Nalasi na Mchoteka

MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti makorongo yaliyotokana na maji ya mvua katika Vijiji vya Nalasi na Mchoteka?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhandisi Fadhili Sandali Chilombe, Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kusini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua changamoto za makorongo katika maeneo mengi nchini ikiwemo katika Vijiji vya Nalasi na Mchoteka vilivyopo katika Halmashauri Tunduru.

Makorongo haya yanasababishwa na mvua zinazoendelea kunyesha na shughuli za kibinadamu za machimbo ya madini ya ujenzi ikiwemo mchanga na kokoto ambazo kwa namna moja au nyingine zimesababisha madhara katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na hali hiyo. Katika mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 10 katika Halmashauri ya Tunduru kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za udhibiti wa mmomonyoko wa udongo na makorongo katika Wilaya ya Tunduru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kuendeleza uelekezaji na uboreshaji wa njia za maji *(drainage systems)* ili kuzuia maji kusambaa hovyo; upandaji wa miti na nyasi za kudhibiti mmomonyoko wa udongo katika maeneo hatarishi; na kutoa elimu kwa jamii kuhusu utunzaji wa mazingira na mbinu za kuzuia mmomonyoko wa udongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira pamoja na kuandaa mipango bora ya matumizi ya ardhi katika maeneo ya miji na vijijini kote nchini. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Engineer* Fadhili Chilombe, swali la nyongeza.

MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri yaliyotolewa na Serikali, lakini uwepo wa makorongo hayo na ukubwa wake limekuwa ni jambo hatarishi sana kwa wakazi wa maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la nyongeza ni kwamba je, Serikali haioni haja ya kuharakisha kuyadhibiti makorongo yao kwa sababu sasa hivi kadri siku zinavyozidi kwenda yanazidi kuongezeka na yanazidi kusogelea makazi ya watu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili; je, kwa ukubwa uliopo wa makorongo yale kusema tuiachie halmashauri peke yake, sioni kama wanaweza. Waziri atakuwa tayari kuambatana na mimi pamoja na wataalam kutoka Serikalini ili tukaone mazingira halisi na itakayowezesha viongozi hawa kuweza kupata nafasi bora ya kujua ni namna gani ya kuyadhibiti haya makorongo?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa Tunduru Kusini, Mheshimiwa *Engineer* Fadhili Sandali Chilombe kwa ufuatiliaji na tunafahamu kwamba makorongo haya yanahatarisha pia maisha ya watoto pale ambapo maji yanakusanyika wakati wa msimu wa mvua na watoto mara nyingine kupata ajali kwenye makorongo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tumetenga fedha shilingi milioni 10 kwa ajili ya kutekeleza utaratibu wa kuanza kuyafukia makorongo yale kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumsisitiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Tunduru kwamba makorongo yale yaliyotokana na uchimbaji wa kifusi kwa ajili ya ujenzi wa barabara za *TANROADS, TARURA* na kadhalika, wanaweza wakaweka utaratibu wakati wanazoa taka katika mji, katika maeneo yale taka ambazo si hatarishi, waendelee kuya-*backfill* yale makorongo taratibu na baada ya muda makorongo yale yatapungua, lakini na Serikali itaendelea kutenga fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunatambua kwamba ni makorongo hatarishi na tumetenga fedha kama awamu ya kwanza kuanza taratibu za kuyafukia na tutaendelea kufanya hivyo kwa awamu, lakini pili, niko tayari kuambatana na wewe ili kuweza kwenda katika Jimbo la Tunduru Kusini kukagua miradi ya

maendeleo na kuhamasisha pia shughuli za maendeleo kwa wananchi wa Tunduru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Emmanuel Khambay, swali la nyongeza.

MHE. EMMANUEL J. KHAMBAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali kwa kutupa kibali cha kutangaza zabuni ya barabara ya kona ya Mrara – Mamire - Ikulu na mkandarasi amepatikana na amefanya *mobilization,* amekwenda pale ameanza kutindua daraja na daraja lile sasa hivi limekuwa ni hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itatoa fedha ili mkandarasi aliyeondoka *site* aweze kurudi *site* kwa sababu daraja limetinduliwa na ni hatarishi hata kwa wananchi, lakini ikumbukwe Babati ni njia panda, hata viongozi wa kitaifa wanapotaka kupita pale walau waende Ikulu, kunawa mikono hawawezi kwenda na viongozi wangu wa Serikali wameniambia hawataruhusu viongozi wa kitaifa kwenda kwenye *rest house* ya Babati kutokana na changamoto hiyo. Ninaomba majibu ya Serikali.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa Babati Mjini, Mheshimiwa Khambay na nimhakikishie tu kwamba tunafahamu kwamba yuko mkandarasi ambaye alipewa kazi ya kujenga barabara na daraja hilo lakini taratibu za malipo huwa zina hatua zake.

Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie kwamba nitafuatilia baada ya kipindi hiki cha Maswali na Majibu, niweze kujiridhisha *certificate* zake au hati za malipo alizowasilisha zimefikia hatua gani ili aweze kulipwa mapema iwezekanavyo na kurejea kukamilisha ujenzi wa daraja hilo muhimu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, swali la nyongeza.

MHE. PROF. JOYCE L. NDALICHAKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Kasulu Mjini mvua ambazo zimenyesha zimesababisha makorongo makubwa na barabara nyingi zimeharibika ikiwemo Barabara ya Murufiti - Shunguliba, Barabara ya Kabanga - Muganza, Heru Juu, Munyegera. Je, ni lini Serikali itatengeneza barabara hizo?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimpongeze sana Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, Mbunge wa Jimbo la Kasulu Mjini kwa ufuatiliaji wake wa mara kwa mara kuhusiana na miundombinu ya barabara, lakini pia na miradi mingine ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tumetangaza 60% ya miradi ya barabara na ninaamini barabara ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja, baadhi lazima zitakuwa kwenye *package* hiyo ambayo tayari imeshatangazwa, ambacho tunakifanya sasa ni kuhakikisha kwamba tunaongeza kasi ya kuwapata makandarasi ili waende *site* kujenga na kurekebisha barabara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafuatilia na nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, kumwelekeza Meneja wa TA*RURA* wa Wilaya ya Kasulu, lakini pia wa Mkoa wa Kigoma kuhakikisha wanazi-*note* barabara ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja na kwa umuhimu wa barabara hizo wazipe kipaumbele kwenye zabuni ambazo zinatangazwa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwita Waitara, swali la nyongeza.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Jimbo la Tarime Vijijini lilitenga fedha kupitia *CSR,* 60% na fedha kutoka Serikali Kuu na wakandarasi wakapatikana Kata za Bumera, Susuni, Ganyange, Nyakonga na Muriba. Mheshimiwa Naibu Waziri unaweza kunisaidia; ni kwa nini fedha zipo, wameenda *site,* wametifua barabara halafu wakaondoka? Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa mujibu wa taratibu na sheria zetu, mkandarasi akishasaini mkataba na kuoneshwa *site* anatakiwa kutekeleza majukumu yake na kuhakikisha kwamba amekamilisha ile kazi kwa mujibu wa mkataba. Sasa ikiwa kuna wakandarasi ambao tayari wamelipwa na wamekabidhiwa *site* za ujenzi wa barabara kwenye kata ambazo Mheshimiwa Mbunge Waitara amezitaja, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tutafuatilia haraka iwezekanavyo mkandarasi mmoja baada ya mwingine na kujiridhisha kwa nini hawaendelei na utekelezaji wa miradi hiyo na ikiwa wamevunja mikataba, tutachukua hatua kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

MHE. MARIAM M. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza, lakini na mimi kipekee nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jinsi anavyopambana hapa Bungeni kujibu maswali yetu vizuri sana, anatukonga nyoyo zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Mkurugenzi wangu wa Halmashauri ya Temeke kwa jinsi anavyopambana katika kufuatilia mapato ya ndani na kufanyia kazi ya kuleta maendeleo, lakini changamoto ya makorongo ipo katika Jimbo

la Temeke, maeneo ya Tambukareli, Mtoni Unguja, lakini na Kilimahewa katika maeneo ya Nyambwela.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga hata ngazi za zege ili wananchi wale ambao wamepitiwa na makorongo haya ya mvua waweze kupata njia ya kupita?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nimpongeze sana mama yangu, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mbunge wa Jimbo la Temeke kwa ufuatiliaji na nimhakikishie tu kwamba Serikali inatambua kwamba tuna changamoto ya baadhi ya barabara zikiwemo barabara ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja za Jimbo la Temeke kuharibiwa sana na mvua ambazo zimenyesha msimu uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwanza tulishafanya tathmini ya barabara zote muhimu sana za kipaumbele ambazo zimeharibika na tayari tunaendelea na taratibu za kuanza kupeleka wakandarasi kwa ajili ya matengenezo. Wakati tunafanya hilo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutatoa kipaumbele katika barabara hizo ambazo zimeharibika vibaya ili ziweze kutengenezwa na kurejesha mawasiliano kwa wananchi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Japhael Lufungija, swali la nyongeza.

MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, barabara za Jimbo la Ulyankulu, Serikali imefanya kazi kubwa kuzijenga, lakini kutokana na mvua kubwa iliyonyesha, barabara nyingi zimesombwa na maji na kwamba masika inayokuja haziwezi kuendelea. Nini mpango wa Serikali wa kuzirejesha hizo barabara kwenye hali nzuri?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, miongoni mwa barabara ambazo zimeanza kutangaza zabuni katika Wilaya ya Kaliua kupitia *TARURA* katika Mkoa wa Tabora ni pamoja na barabara za Jimbo la Ulyankulu kwa Mheshimiwa Japhael Lufungija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Lufungija kwamba tuko kwenye hatua za kuanza matengenezo, lakini zoezi hili ni endelevu; Serikali itaendelea kutenga fedha mara kwa mara kwa kadri ya upatikanaji wa fedha ili kuhakikisha kwamba tunaboresha barabara zetu, lakini pia kujenga na madaraja na makalvati katika maeneo ambayo yanahitaji miundombinu hiyo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, swali la nyongeza.

MHE. DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Naibu Waziri, changamoto ya makorongo hususani kwa wanawake wa Mkoa wa Njombe imekuwa ni changamoto kubwa. Wanawake hawa wanalima mazao parachichi, viazi na wanahitaji barabara nzuri kwa ajili ya masoko ya bidhaa zao, na eneo la Madilu, Madete, Lugenge, Mundindi, ni eneo ambalo makorongo yako mengi na kumekuwa na changamoto bidhaa ziko nyingi sana, vyakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua Serikali ina mpango gani wa kuboresha maeneo haya katika Wilaya ya Ludewa?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nimpongeze sana dada yangu, Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Njombe kwa uchapakazi wake, kwa hakika amekuwa Mbunge rahim, mfuatiliaji sana, na mimi

nikuhakikishie kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI tutaendelea kukupa ushirikiano wewe kama Mbunge wa Viti Maalum, lakini na wananchi wa Mkoa wa Njombe na Watanzania kwa ujumla, kuhakikisha miundombinu ya barabara inaboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu kwamba katika Wilaya ya Ludewa kuna changamoto ya baadhi ya barabara za Mundindi na nyingine ambazo amezitaja. Nimhakikishie kwamba kwanza Serikali imeshaweka mpango kwa ajili ya kwenda kurekebisha barabara zote muhimu kipaumbele ambazo zimeathirika na mvua, lakini pili tutaendelea kutenga fedha kwenye bajeti zetu mara kwa mara ikiwemo bajeti ya dharura na bajeti ya kawaida kuhakikisha kwamba barabara hizo zinajengwa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, katika Jimbo la Hai kuna makorongo korofi manne makubwa. Moja ni lile la Uroki, Barabara ya Uswaa kwenda kwa Sadala, lakini lingine ni la Narumu kwa maana ya kupita Narumu kwenda Mfoni; na lingine ni la Vijana kwa maana Barabara ya Mbohera kwenda Vijana na Urukunungu. Haya yamekuwa ni korofi kweli kweli.

Je, ni lini sasa Serikali itajenga kama ilivyojenga ile ya kutoka Kalali kwenda Muronga ili barabara hizi ziweze kutumika na ziweze kusafirisha mazao kwa kipindi hiki cha msimu?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya vipaumbele vya Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)* ni kuhakikisha tunaondoa vikwazo vikubwa vinavyosababisha barabara zetu zisipitike, yakiwemo makorongo makubwa katika barabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kwanza nimpongeze Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Jimbo la Hai kwa ufuatiliaji kwa manufaa ya wananchi wa jimbo hilo, lakini pili, nimwelekeze Meneja wa *TARURA* wa Wilaya ya Hai, wafike kwenye makorongo hayo kwa Vijana na maeneo mengine kwa Sadala, wafanye tathmini kiasi gani cha fedha kinahitajika tuwe na mpango mahususi wa kwenda kuyatengeneza na kudhibiti changamoto ya makorongo katika maeneo hayo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Engineer* Johnston Mutasingwa, swali la nyongeza.

MHE. ENG. JOHNSTON J. MUTASINGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kazi nzuri wanazozifanya, Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo letu la Bukoba Mjini kuna makorongo makubwa sana katika Kata ya Hamugembe, tuna korongo moja kubwa sana ambalo linatokana na mvua zinazonyesha. Katika Kata yetu ya Rwamishenye, tuna korongo kubwa sana ambalo linahatarisha sana makazi ya watu na hata usalama wa watoto wadogo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuyajengea haya makorongo makubwa yanayotokana na mvua zinazoendelea kunyesha nchini? Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, katika barabara zetu makorongo ni changamoto ambayo inahitaji utatuzi wa haraka. kwa hiyo ninaomba nimpongeze Mheshimiwa *Engineer* Johnston, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Mjini, lakini nitumie nafasi hii kumhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafuatilia kuona ikiwa makorongo hayo yako

kwenye barabara zetu, tuweze kufanya na kuchukua hatua za haraka iwezekanavyo ili tuweze kuyafukia na kudhibiti barabara zetu ziweze kupitika vizuri. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Edifonsi Kanoni, swali la nyongeza.

MHE. EDIFONSI J. KANONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza. Kwanza nimshukuru na nimpongeze Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Rukwa, lakini Meneja wa *TARURA* Wilaya ya Kalambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Katazi kwenda Ninga barabara imekatika haipitiki kutokana na hali ya mvua, lakini barabara ya kutoka Ulumi kuelekea Kalepula nayo haipitiki, lakini barabara ya Ulumi kuelekea Mnamba haipitiki kutokana na changamoto za mvua zina makorongo makubwa na ukizingatia sasa ni msimu wa kilimo ambapo wananchi wanategemea kupata barabara nzuri kwa ajili ya kuboresha biashara zao za mazao.

Je, nini mpango wa Serikali kutenga bajeti kuhakikisha kwamba hizi barabara zinaimarika? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimhakikishie Mheshimiwa Kanoni, Mbunge wa Jimbo la Kalambo, mpango wa Serikali kwanza ni kuhakikisha kwamba barabara hizi zote zinafanyiwa matengenezo na ndiyo maana tayari tumeshatangaza 60% ya bajeti zetu za mwaka kwa ajili ya kupata makandarasi ili wafike katika barabara zote muhimu na kipaumbele katika halmashauri zetu ambazo zimeathirika, waweze kuzitengeneza kuhakikisha kwamba wanarejesha shughuli za mawasiliano.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutahakikisha barabara hizo tunazifanyia matengenezo mapema

iwezekanavyo kwa awamu ili kuondoa changamoto ya usafiri kwa wananchi wa Kata hizo zote. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuzuia maafa kwa kutumia gharama ndogo sana kuliko kushughulikia maafa pale ambapo unakuta yanatokea na kwa kuwa katika Jimbo la Tarime Mjini, kuna korongo la Starehe ambalo ni hatarishi. Tumekuwa tukitengewa fedha, lakini halijengwi kingo ili kuweza kuzuia mmomonyoko ambao unaenda kwenye nyumba za wananchi.

Sasa nataka kujua Serikali ina mpango gani mahususi wa kuingilia kati korongo hili ili kuweza kulijenga na kuweza kuondoa uhatarishi wa usalama wa maisha ya wananchi, kwa sababu sasa hivi nyufa zile zimeenda mpaka kwenye nyumba za wananchi na kuweza kuhatarisha usalama wa mali na uwekezaji wa wananchi wa Mtaa wa Starehe?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimhakikishie Mbunge wa Jimbo la Tarime Mjini, dada yangu Mheshimiwa Esther Matiko, kwamba moja ya vipaumbele vya Serikali ni kuhakikisha tunaondoa maeneo hatarishi katika barabara zetu yakiwemo makorongo, lakini pia na athari za makorongo kupeleka mafuriko kwa wananchi. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakwenda kufanya tathmini ya kwa nini hilo korongo linajengwa, lakini halijengewi kingo ili tujenge kingo, tuweze kudhibiti changamoto hiyo isijirudie mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, nimwelekeze Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Mara pamoja na Wilaya ya

Tarime wafike eneo hilo, waone kwa nini mara kwa mara tukifanya ujenzi linafunguka, linapasuka tena, lakini linapeleka maji kwa wananchi ili tuje na *design* nzuri baada ya usanifu makini ili tuweze kudhibiti kabisa changamoto ya korongo hilo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yustina Rahhi, swali la nyongeza.

MHE. YUSTINA A. RAHHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na mimi kunipa nafasi ya swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna makorongo makubwa na ya hatari katika Mkoa wa Manyara hususani korongo la Gunyoda yaliyosababishwa na matetemeko na mvua.

Sasa je, Serikali ina utaratibu upi mahususi wa kujenga Kamati za Mazingira katika ngazi ya kata na labda ya kijiji kudhibiti makorongo hayo?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum, Manyara amesema vizuri kwamba Serikali imeendelea, kwanza kuziboresha Kamati za Mazingira katika ngazi za vijiji, ngazi za kata na ngazi za wilaya kuhakikisha kwamba katika maeneo yao wanadhibiti uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba pamoja na taratibu za kurekebisha makorongo hayo, lakini Serikali itaendelea kuhakikisha Kamati za Mazingira zinatimiza majukumu yao kwa wakati ili kuendelea kuzuia madhara ambayo yanatokana na makorongo ambayo yanatokea mara kwa mara.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili linafanyika na Serikali na tutaendelea kusisitiza kuhakikisha kwamba kamati zile zinakuwa na nguvu zaidi lakini pia zinatimiza majukumu yao ipasavyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, Naibu Waziri TAMISEMI, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea, sasa ni Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana, namwita Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake.

Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali.

Na. 545

Kuwezesha Vikundi vya Vijana na Wenye Mahitaji Maalum

MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha vijana wenye vikundi vilivyosajiliwa pamoja na wenye mahitaji maalum?

MWENYEKITI: Majibu, Naibu Waziri Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, kwa niaba.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutekeleza mpango wa muda mrefu wa kuwawezesha vijana, wakiwemo wenye mahitaji maalum kupitia vikundi vilivyosajiliwa ili kuimarisha ushiriki wao katika shughuli za kiuchumi na maendeleo ya Taifa. Uwezeshaji huo unahusisha utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, Programu ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi inayotekelezwa kupitia shilingi bilioni 200 za ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na mikopo inayotokana na 10% ya mapato ya ndani ya halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali inaendelea kutekeleza utaratibu wa kutenga 30% ya zabuni za umma kwa makundi maalum, kuunganisha vikundi vya vijana na taasisi za kifedha na kuimarisha mifumo ya uratibu na taarifa ili kuongeza fursa za ajira, ujasiriamali na maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Latifa Juwakali, swali la nyongeza

MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Pia, naishukuru Serikali kupitia Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa kila Mkoa wa nchi hii una rasilimali muhimu na ya kipekee. Mimi binafsi leo ukiniambia Mkoa wa Geita ninaiona dhahabu, ukiniambia Mkoa wa Mtwara ninaiona korosho.

Je, Serikali haioni namna sasa ya kupitia upya sera na kujipanga ili kuweza kuanzisha miradi ya mfano katika mkoa ili waweze kuwashirikisha vijana wengi katika mikoa mbalimbali na kuweza kushiriki kikamilifu kwa sababu kila mkoa una rasilimali ambayo inajitegemea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kutokana na majibu yako Mheshimiwa Naibu Waziri na mimi binafsi ninafahamu kwamba ipo sheria na sera ambayo inatoa mwongozo moja kwa moja wa kutoa 30% katika manunuzi. Nilikuwa ninataka kufahamu, je, Serikali inatumia njia gani kufuatilia halmashauri na taasisi za umma ambazo hazitekelezi sera hii na sheria hii ya kutenga 30% za manunuzi ya umma kwa ajili ya kuwawezesha vijana, kina mama na watu wa makundi maalum, hasa walemavu? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpa heko Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali kwa mapambano yake yasiyopooza ya kuwapigania vijana wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi hii ndiyo maana ya vijana wa Tanzania wanaendelea kumpa imani na kumrudisha kwenye Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili aendelee kuwapambania. Ninamwombea Mungu asichoke na aendelee kufanya kazi na jukumu alilopewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujibu maswali yake, kwanza tumepokea shukrani zake, kama Serikali tunamshukuru. Kazi kubwa inaendelea kufanyika chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ili kuhakikisha vijana wa nchi hii hawakwami, lakini kuhusiana na *flagship projects* kwa kila mkoa kutokana na rasilimali ambazo zipo katika mikoa hiyo, ni wazo zuri na ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tumelichukua na tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Sheria ya Manunuzi ya Umma Namba 10 ya Mwaka 2023 ambapo kifungu cha 64 kinaelezea wazi ya kwamba taasisi za umma zinalazimika kutenga 30% ya manunuzi yake kwa makundi maalum, makundi ambayo vijana nao wanakwenda kunufaika nayo. Wasiotekeleza kwanza wanaanzisha hoja za kiukaguzi na upo uwezekano wa hata viongozi wa taasisi hizo kufunguliwa mashtaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kufanya juhudi mbalimbali kuhakikisha utekelezaji wa sheria hii unafanyika. Na hata kwenye mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka huu miongoni mwa vigezo vinavyokaguliwa ambavyo vinaweza vikaifanya halmashauri kushinda ni utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali bado inaendelea kukusanya maoni na itaendelea kuhakikisha kwamba inasimamia kutekelezwa kwa sheria hii na kuhakikisha makundi maalum

ambayo Mheshimiwa Juwakali anayasimamia, kwa mfano vijana, yanaendelea kunufaika, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea ninaomba nitangaze na kuwatambulisha kwenu wageni walioko Bungeni asubuhi ya leo.

Tunaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika; wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Fadhili Ally Liwaka ambao ni viongozi wa Chama na Serikali kutoka Wilaya na Nachingwea, Mkoani Lindi, ambapo yupo Mheshimiwa Mohamed Moyo, Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo Mheshimiwa Adinani Mpyagila, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Nachingwea na pia yupo Mhandisi Chionda Mfaume, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Nachingwea. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini ambao ni familia yake kutoka Longido, Mkoani Arusha; yupo Ndugu Agnes Kiruswa, mke wa Mheshimiwa Naibu Waziri na pia yupo Ndugu Zefania Kiruswa, mtoto wa Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni wageni 35 wa Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi ambao Umoja wa Walimu kutoka Tarime, Mkoani Mara. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Devota Mathew Minja, ambaye ni Ndugu Raphael Mrutu, Balozi wa Mazingira Kanda ya Kaskazini kutoka Same, Mkoani Kilimanjaro. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia yupo mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishegoma Kikoyo ambaye ni Ndugu Gregory Kente, mkulima kutoka Muleba Mkoani Kagera. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Charles Mhando Njama ambao familia yake kutoka Wilayani Korogwe, Mkoani Tanga. *(Makofi)*

Pia, wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Charles Mhando Njama ambao ni rafiki zake kutoka Ilemela, Jijini Mwanza. *(Makofi)*

Wapo wageni 17 wa Mheshimiwa Dkt. Emanuel Qambaji Nuwas ambao ni kundi la wazee kutoka Wilaya ya Mbulu na Mkalama, Mkoani Manyara. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Nuwas ambao ni wakulima kutoka Wilaya ya Mbulu, Mkoani Manyara. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia wapo wageni 32 wa Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava ambao ni watumishi na watendaji wa Serikali kutoka Kata ya Mazinde, Wilaya ya Korogwe, Mkoani Tanga. *(Makofi)*

Wapo wageni 67 wa Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako ambao ni wanafunzi na walimu wa Shule ya Msingi ya Jamadel ya Jijini Dar es Salaam. Miongoni mwa hao wanafunzi wapo wajukuu wa Mheshimiwa Profesa Ndalichako ambao ni Amara na Darius. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni 91 wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga ambao ni wanafunzi na walimu wa Shule ya Msingi ya Jubilation ya Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni 26 wa Mheshimiwa Haidary Hemed Sumry ambao ni wanafunzi kutoka Nkasi, Mkoani Rukwa. *(Makofi)*

Pia, wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanafunzi 49 na walimu 10 kutoka *Marangu Hills Academy* ya Mkoani Kilimanjaro. *(Makofi)*

Wageni wetu wote karibuni hapa Bungeni Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, sasa ninamwita Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe, Mbunge wa Viti Maalum aweze kuuliza swali lake.

Na. 546

Uchakataji wa Taka na Matumizi ya Nishati kwenye Hoteli

MHE. LUCY EDWARD MWAKYEMBE aliuliza: -

Je, Serikali kwa kushirikiana na Majukwaa ya Kimataifa na Kamati za Kitaifa itasimamiaje uchakataji wa taka na matumizi ya nishati kwenye hoteli?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi mwanachama wa mikataba mbalimbali ya kuhifadhi mazingira na mabadiliko ya tabianchi ambapo kupitia mikataba hii, Tanzania imekuwa ikishiriki katika mikutano ya kimataifa ya nchi wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mikutano hiyo Tanzania imeendelea kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya uhifadhi wa mazingira ikiwemo udhibiti wa taka. Aidha, kupitia makubaliano ya Paris, Tanzania imeandaa Mpango wa Kitaifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi. Pamoja na mambo mengine, mchango huo umebainisha eneo la udhibiti wa taka kama mojawapo ya vipaumbele vya kupunguza uzalishaji wa hewa ya kaboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Taka wa Miaka Mitano (2025 – 2030) wenye lengo la kuimarisha mfumo wa usimamizi wa taka kwa dhana ya uchumi rejeshi ambapo taka zinazozalishwa zinaweza kutumika tena kama malighafi viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imeendelea kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya usimamizi wa taka hususani taka ozo zinazotoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo hoteli, masokoni na nyumbani. Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya viwanda sita vimeanzishwa kwa ajili ya kuchakata na kurejelesha taka ozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lucy Mwakyembe, maswali ya nyongeza.

MHE. LUCY EDWARD MWAKYEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi zake za kuimarisha sekta ya utalii kupitia filamu ile ya *Royal Tour*, lakini pia, nimpongeze Dkt. Hussein Mwinyi kupitia juhudi zake za kuimarisha uchumi wa buluu kule Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Zanzibar kupitia uchumi wa buluu pamoja na sekta ya utalii ina hoteli zaidi ya 2,000, Je, Serikali ni kwa namna gani itashirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika uhifadhi wa mazingira na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi kupitia uchakataji wa taka za hotelini na matumizi ya nishati safi inayotokana na ushiriki wa majukwaa ya Kimataifa na Kamati za Kimataifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu namba mbili, kwa kuwa janga la mabadiliko ya tabianchi linagusa nchi zote, watu wote, jamii zote na wa hali zote (wenye kipato na wasiokuwa na kipato), je, Serikali imechukua hatua gani za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika kujenga ustahamilivu na uendelevu? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Lucy Edward Mwakembe kwa namna ambavyo anawawakilisha vyema kundi la wafanyakazi ndani ya nchi yetu na Watanzania wa pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimekuwa zikishirikiana katika kutafuta fedha kupitia majukwaa haya ya kimataifa kwa ajili ya udhibiti na uhifadhi wa mazingira. Vilevile Serikali hizi mbili zimekuwa zikiendesha kampeni ya pamoja kwa ajili ya kuhamasisha matumizi ya nishati safi na salama, na hasa hasa kwenye taasisi zote ambazo zinahudumia watu zaidi ya 100 tunafanya kampeni kuhakikisha taasisi hizo zinatumia nishati safi na salama ikiwemo nishati kama ya gesi na jambo hili limemfanya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa ni *champion* ndani ya nchi yetu, ndani ya Afrika Mashariki na ndani ya dunia kama *champion* namba moja wa uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo tu hivyo, lakini Serikali zetu zimeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi ili kuwekeza katika biashara ya uchakataji wa taka ziweze kutumika tena na hivyo kupelekea kuhifadhi mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwenye suala hili la ushirikiano, Taasisi yetu ya Uhifadhi na Utunzaji wa Mazingira *(NEMC)* upande wa Tanzania Bara pamoja na Taasisi ya Utunzaji wa Mazingira kule Zanzibar *(ZEMA)* zimesaini makubaliano ya pamoja *(MOU)* kwa ajili ya ushirikiano kubadilishana uzoefu na kushirikiana kwenye masuala mbalimbali ya uhifadhi ikiwemo uchakataji wa taka. Makubaliano haya kwa sasa yako Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kufanyiwa *vetting. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili la nyongeza ametaka kujua hatua ambazo Serikali inachukua ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Hatua ya kwanza na ambayo imekuwa endelevu ni utunzaji wa misitu na kupanda miti kwa ajili ya kuimarisha misitu yetu iliyopo na kupanda misitu mingine mipya maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea na utunzaji wa vyanzo vya maji katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu ili kuhakikisha kwamba mazingira yetu na vyanzo hivyo yanakuwa himilivu. Vivyo hivyo, Serikali tumekuwa tukihamasisha sana habari ya kilimo himilivu, kilimo ambacho kinazingatia kutoharibu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeendelea kusimamia na kudhibiti uzalishaji wa taka kwa kutumia sheria zilizopo na kuzisimamia barabara ili watu wote wayatunze mazingira kama ambavyo tunatamani iwe, na mwisho tumeendelea na matumizi ya nishati safi na salama na pamoja na utekelezaji wa miradi ya kijamii ya uhimilivu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, sasa namwita Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka, Mbunge wa Tanga, aweze kuuliza swali lake.

Na. 547

Ujenzi wa Barabara ya Soni – Bumbuli hadi Dindira

MHE. KASSIMU A. MBARAKA aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Soni - Mbelei, Kwalei – Kwehangala - Bumbuli hadi Dindira kilometa 74 kwa kiwango cha lami?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka, Mbunge wa Tanga Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Soni – Mbelei – Kwalei – Kwehangala - Bumbuli hadi Dindira yenye urefu wa kilometa 74 ni barabara ya mkoa inayohudumiwa na *TANROADS* Mkoa wa Tanga. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika na taratibu za kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami zitafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza itahusisha ujenzi wa kilometa 9.3 kutoka Kwameta hadi Kwashemshi ambapo zabuni za kumpata mkandarasi zipo katika hatua ya tathmini *(evaluation)*. Aidha, awamu ya pili itahusisha ujenzi wa kilometa 22 kutoka Soni hadi Bumbuli ambapo zabuni ya kumpata mkandarasi inatarajiwa kutangazwa mwishoni mwa mwezi Juni, 2026. Baada ya mkandarasi wa ujenzi kujulikana na mkataba kusainiwa, kazi za ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami zitaanza, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kassimu Mbaraka, swali la nyongeza.

Waheshimiwa Wabunge, mliowasha *microphones* tafadhali tuzime kwa sababu muuliza swali amewasha.

MHE. KASSIMU A. MBARAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa barabara hii imo kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi muda mrefu na ni barabara ambayo imekuwa ikiahidiwa sana, je, Mheshimiwa Waziri anaweza akawa tayari baada ya Bunge hili kuisha kuhakikisha kwamba anaenda kutuahidi na kutueleza

haya yaliyotueleza hapa Bungeni mbele ya wananchi wa eneo hili la Mombo pamoja na eneo hili linaloelekea Bumbuli? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, je, ni upi mpango wa Serikali sasa kuitanua Barabara ya Mombo – Soni - Lushoto kwa sababu *feasibility study* zilishafanyika, sasa mpango ni upi kuitanua barabara hii iweze kupitika vizuri? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia barabara za Mkoa wa Tanga zikiwemo hizi barabara ambazo zinakwenda makao makuu ya Wilaya ya Lushoto, lakini pia kule Bumbuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba niko tayari kutembelea barabara hii na kuwaeleza wananchi hiki ambacho Serikali imekisema leo kwa sababu ni kweli kwamba hii barabara kimsingi ilishatangazwa lakini katika majadiliano na mkandarasi Serikali iliona gharama ni kubwa na ndiyo maana tunapotangaza hapa ni kutangaza kwa mara ya pili. Kwa hiyo, tutatangaza tena, lakini tuna hakika hii barabara ni moja ya barabara kipaumbele sana kuanza kuijenga hizo kilometa 22 kutoka Soni hadi Bumbuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuipanua Barabara ya Mombo – Soni – Lushoto, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, Serikali tulishaona hii barabara ilijengwa kipindi cha nyuma sana, ni nyembamba sana na ni barabara ambayo inapitisha magari mengi, makubwa na mazito na ndiyo maana tayari tumeshafanya usanifu na Serikali tuko tunatafuta fedha ili wakati wowote tutakapokuwa tumepata fedha..., kwa sababu ni barabara ambayo iko kwenye miinuko mikali sana, tukipata fedha za uhakika basi hiyo barabara tuanze kuijenga ikiwa ni pamoja na kuipanua ili iende na vipimo vya sasa kwa barabara ambazo tunazijenga. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Timotheo Mnzava, swali la nyongeza.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwanza niishukuru Serikali kwa kazi nzuri ambayo imefanyika kuanzia jana kwenye lile eneo la Kumba kwenye barabara ile ya Mashewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali dogo tu; kama ilivyo kwa barabara hii ya Soni, iko ahadi ya muda mrefu ya barabara kutoka Korogwe kwa maana ya *Old Korogwe* – Kwamndolwa – Mabokweni, na tofauti na barabara hii ya Soni, barabara hii tayari usanifu ulikamilika na zabuni ilishatangazwa siku nyingi na naamini mkandarasi alishapatikana. Ni lini kazi ya ujenzi wa lami wa barabara hii itaanza? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Barabara hii ni barabara ndefu ambayo inatoka Korogwe kwenda Mabokweni na barabara hii tutaanza kuijenga kwa awamu, kwanza kuanzia Korogwe kwa kilometa 10, lakini pia kutoka pale Maramba mpaka Kijiji cha Mtapwa kilometa 10 ambapo tunavyoongea sasa hivi ile mikataba iko kwa mwanasheria kwa ajili ya kufanyia *vetting*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna uhakika kadri tunavyotafuta fedha, lengo ni kuikamilisha ile barabara yote muhimu kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo, swali la nyongeza.

MHE. DKT. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Kisarawe – Mpuyani – Maneromango kilometa 54 ambayo naishukuru Wizara wameshaitangaza barabara ile na tarehe 15 Julai, 2025 mkandarasi aitwaye *Sethpro Uganda Limited* alipewa *notification* ya barabara hiyo na bahati nzuri wiki sita

zilizopita, nimshukuru sana Waziri wa Ujenzi alikuwa Kisarawe na akatoa wiki mbili kuhakikisha taratibu za mikataba zinakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile sasa hivi wiki sita zimeshapita, sasa naomba kujua ni lini mkandarasi yule ataingia *site* kujenga kile kipande cha kilometa 34.5 ambacho kilitangazwa? Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Jafo, Mbunge wa Kisarawe na namhakikishia kwamba tunachofanya sasa hivi tuko kwenye maandalizi ya kuandaa malipo ya kumlipa huyo mkandarasi ili aweze kwenda *site* na kuanza kufanya hiyo kazi. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Engineer* Ramadhani Singano, swali la nyongeza.

MHE. RAMADHANI H. SINGANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Barabara ya Soni – Bumbuli uboreshaji wake lazima utaathiri *stand* ya Soni ambayo kwanza ni finyu. Serikali katika upembuzi yakinifu imezingatia upanuzi wa *stand* hii wakati inafikiria kurekebisha Barabara ya Soni – Bumbuli - kilometa 22?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijamsikia vizuri hapa mwishoni amesema Serikali ina..., sijamsikia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa *Engineer* arudie.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tunaomba tupunguze kidogo sauti ili mwuliza swali na mjibu swali waweze kusikilizana.

Mheshimiwa *Engineer* Ramadhani Singano.

MHE. RAMADHANI H. SINGANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa mara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji wa barabara ya Soni – Bumbuli lazima utaathiri *stand* ndogo ya Soni ambayo bado ni finyu kwa sababu ndiyo *stand* ya magari ya kwenda mikoani. Sasa upembuzi yakinifu umezingatia upanuzi wa *stand* hii ambayo itaathirika au *stand* mbadala?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na bahati nzuri ni mhandisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana kunakuwa na hatua mbili; kuna suala la upembuzi yakinifu ambao kazi yake kubwa ni kuangalia yale mahitaji yote ya jamii lazima yazingatiwe wakati unafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, tunapata taarifa za kitaalamu barabara itajengwaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba vitu vyote ambavyo vinaathirika kwa sababu ya kujenga hiyo barabara vitafikiriwa na kuhakikiwa kwamba viko kwenye mpango wa ama kuihamisha ama kuiboresha ama kuilipa fidia na ndiyo maana ya hizo hatua mbili, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba hivyo vyote vimezingatiwa wakati wa kufanya shughuli ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Aysharose Mattembe, swali la nyongeza.

MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ujenzi wa barabara inayoanzia Sepuka – Ndago – Kizaga ni barabara muhimu sana

kwa maendeleo ya Jimbo la Ikungi na Iramba, lakini ujenzi wake kwa kiwango cha lami umekuwa unasuasua.

Je, ni lini sasa Serikali itapeleka fedha za kutosha ili kukamilisha ujenzi wa barabara hii? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii tulishaanza kujenga na mkandarasi alishapatikana ikiwa ni pamoja na kuanza kujenga kambi ya mkandarasi, lakini pia kambi ya mhandisi mshauri. Ni moja ya barabara ambazo wakandarasi tuko tunawaandalia fedha za kwanza kukamilisha yale malipo ya awali na kulipa zile hati zao za mwanzo za malipo ili sasa waweze kushika kasi ya kujenga hizi barabara ikiwa ni pamoja na hiyo Barabara ya Sabasaba – Ndago – Kizaga. Ahsante.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, sasa ninamwita Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Lupembe, aweze kuuliza swali lake.

Na. 548

Ujenzi wa Barabara ya Kibena hadi Madeke Kilometa 126

MHE. EDWIN E. SWALLE aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara kutoka Kibena hadi Madeke kilometa 126 kwa kiwango cha lami?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Lupembe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Kibena – Lupembe – Madeke yenye urefu wa kilometa 126.18 umegawanywa katika sehemu kuu tatu za utekelezaji zinazohusisha Kibena – Kidegembye, kilometa 41.95, Kidegembye – Mfiriga, kilometa 40 na Mfiriga – Madeke, kilometa 42.02. Kwa sasa taratibu za ununuzi wa mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya Kibena – Kidegembye yenye urefu wa kilometa 41.95 zipo katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa sehemu zilizobaki za Kidegembye – Mfiriga, kilometa 40 na Mfiriga – Madeke, kilometa 42.02 utekelezaji wake utategemea upatikanaji wa fedha. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Edwin Swalle, swali la nyongeza.

MHE. EDWIN E. SWALLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, naishukuru sana Serikali kwa kuanza kutoa kipaumbele kwenye hii barabara muhimu sana ya Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Morogoro. Kwa kuwa kwenye majibu ya Serikali wanasema wapo kwenye hatua za mwisho za kukamilisha hatua za mzabuni kwa maana ya *tender* ya ujenzi wa hii barabara, wananchi wa Lupembe wamekuwa wakisubiri kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara imekuwa na maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwamba ianze ujenzi. Ningetamani kujua kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Lupembe, ni lini hasa mkataba huu unasainiwa na kuanza ujenzi wa kilometa za kwanza za hii barabara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwenye hii Barabara ya Kibena – Lupembe – Madeke, yako maeneo ambayo wananchi walipisha kwa ajili ya huu mradi. Sehemu kama za Nyombo, Kidegembye, Matembwe, Wanginyi, Lupembe, Mfiriga mpaka Madeke, wameacha maeneo kwa ajili ya huu mradi, lakini hawajalipwa fidia na tathmini ilishafanyika. Wananchi hawa

wanapewa fidia yao lini ili mradi uanze ujenzi wa hii lami ya wananchi? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni kwamba sisi kama Wizara ya Ujenzi tumeshakamilisha taratibu zote za kiufundi na tunavyoongea sasa hivi kama alivyosema hii ilikuwa ni ahadi ya Rais kuanza kujenga kipande hicho cha barabara kilometa takribani kama 42 ama 41 na *point*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tumesema tuko kwenye hatua za mwisho za manunuzi na tunaposema hatua za mwisho, kila kitu kimeshakamilika. Sasa hivi tunaongea na wenzetu wa Wizara ya Fedha ili tutakapopata tu hizo fedha tuweze kumlipa mkandarasi fedha ya awali aweze kuanza kazi, ndicho kitu kilichobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ndiyo maana tunasema tuko kwenye hatua za mwisho, atakapokuwa analipwa hiyo fedha basi anaanza hiyo kazi kuifanya. Kwa hiyo, tuko tayari tumeshapeleka gharama kwa wenzetu wa fedha waweze kutoa hiyo fedha tuanze ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wananchi ambao watapisha ujenzi wa hii barabara, kama alivyosema mwenyewe, tulishakwenda, tulishafanya tathmini ya nani atalipwa na jedwali liko Wizara ya Fedha. Nimhakikishie hatutaanza kujenga barabara kabla ya wananchi hawa ambao wamepisha barabara hatujawalipa. Kwa hiyo, vitu vyote vitakwenda pamoja, wakati tunaanza barabara tunahakikisha kwanza wale waliopisha barabara wanalipwa fidia halafu ndiyo tunaanza ujenzi wa hiyo barabara. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Agnes Marwa, swali la nyongeza.

MHE. AGNES M. MARWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Musoma - Busekela ndiyo barabara kubwa ya kiuchumi Musoma Vijijini. Katika barabara hii kuna madaraja ambayo ni

hatarishi, Daraja la Nyasaungu na Daraja la Suguti. Je, Serikali ni lini itatujengea madaraja haya mawili ya Suguti na Nyasaungu ili angalau tupite vizuri hata kwenye barabara yetu hiyo ya vumbi? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niseme tu hii barabara ni kweli barabara muhimu, barabara ya uchumi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwanza tumeshatangaza kuanza kilometa 40 za hii barabara na tumetenganisha, hayo madaraja nayo yatakuwa na utaratibu wake kuyajenga kwa sababu tuliona tukiyaunganisha pamoja gharama inaweza ikachukua muda. Kwa hiyo, tunafahamu ili tuweze kwenda haraka basi hayo madaraja pia yatajengwa kwa utaratibu tofauti na hizi kilometa 40 ambazo tumezitangaza.

Kwa hiyo, tunajua barabara hiyo ni muhimu, madaraja hayo ni muhimu, kwa hiyo tunakwenda kuvijenga vyote ikiwa ni pamoja na hizo kilometa 40 ambazo tumeshazitangaza tayari. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Clayton Chipando, swali la nyongeza.

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Jimbo la Kigoma Mjini kuna *two-way* ambayo imejengwa na *TANROADS,* lakini tatizo kubwa lililopo kwenye ile *two-way* ni *u-turn,* inamlazimu mwananchi anayetoka Mwanga ili avuke upande wa pili wa Katubuka inamlazimu kutembea kilometa mbili kutafuta *u-turn*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza *u-turn* ili kuwasaidia wakazi wa Mwanga na maeneo mengine wakitaka kwenda Katubuka, *airport* waweze kupata sehemu nzuri ya kuweza kukunjia? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi miundombinu na hasa miundombinu ya kisasa ni kurahisisha mawasiliano ama kutembea katika miji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mwakilishi wa Wana-Kigoma ameona kuna changamoto ya *u-turn*, nataka tu nitoe maelekezo hapa kwa Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Kigoma, lakini pia na watu wanaohusika na *design* wa makao makuu waweze kwenda Mkoa wa Kigoma, waangalie hiyo *u-turn* ikiwa ni pamoja na kupata pengine mawasiliano na Mheshimiwa Mbunge husika kuona namna ya kurahisisha *u-turn* ambayo tunaamini hatujengi barabara ili ziweze kuleta changamoto, tunajenga barabara ziweze kurahisisha namna ya magari kutembea mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge nimhakikishie tumelichukua na tutakwenda kuliangalia kama mazingira yapo ya kurahisisha zaidi hiyo *u-turn* ambayo ameiomba. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Devota Minja, swali la nyongeza.

MHE. DEVOTA M. MINJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Morogoro ni miongoni mwa mikoa yenye barabara mbovu sana. Barabara ya Ifakara – Mlimba, Barabara ya Ifakara – Ulanga – Malinyi, Barabara ya Bigwa – Kisaki; kumekuwa na ahadi nyingi sana za Serikali za kujenga barabara hizi. Je, ni lini Serikali itatekeleza? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na mheshimiwa Mbunge, Morogoro ni kati ya mikoa ambayo kwanza ina mvua nyingi na inapokea maji mengi kutoka mikoa ya bara kupita. Kwa hiyo ni mikoa ambayo inaathirika sana hasa kipindi cha mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe tu taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba tunavyoongea sasa hivi tuna mpango wa kujenga kwanza kwa awamu kwenye swali la msingi, hii barabara ya Ifakara – Mlimba – Kibena ndiyo hiyo barabara ambayo Njombe tumeanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanza na kilometa 40 lakini kuanzia Morogoro kilometa 100. Kuanzia Ifakara kuelekea Mlimba tuna wakandarasi wawili ambao tayari tumeshawapata ili waweze kuanza kujenga hiyo barabara ninadhani tutakuwa tumepunguza sana hiyo changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bigwa – Kisaki tunaanza na kilometa kama sikosei ni kilometa 78 ambazo tunakwenda mpaka Mvuha tayari tumeshapata mkandarasi anaanza kujenga ikiwa ni kwenda kuifikisha Masaki, lakini Ifakara – Lupiro – Mahenge lakini sisi tunakwenda kwanza Malinyi kilometa 112 tayari tumeshapata mkandarasi anasubiri kulipwa fedha ya awali ili kuanza sasa kupunguza changamoto ambazo zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika kwa hizo barabara zote tatu tulizozipata tayari Serikali imeshaanza utekelezaji wa kuziboresha ikiwa ni kuzijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya, Naibu Waziri wa Ujenzi, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo sasa namwita Mheshimiwa Devotha Daniel, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake na kwa niaba, Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule, aulize swali hilo.

Na. 549

Kuboresha Kilimo Mkoa wa Kagera

MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE K.n.y. MHE. DEVOTHA M. MBURARUGABA aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kubadilisha kilimo Mkoani Kagera kutoka kilimo cha kujikimu kwenda kilimo cha viwanda na kuongeza thamani ya mazao?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Serikali inaendelea kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji na tija ya mazao ya kilimo nchini ikiwemo Mkoa wa Kagera ili kuongeza upatikanaji wa malighafi za viwandani. Katika kufanikisha hilo, Wizara imeendelea kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima, kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mabwawa manne na skimu 14 zenye ukubwa wa hekta 19,000 yatakayonufaisha wakulima takribani 30,500 na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika Bonde la Mto Ngono litakalonufaisha wakulima takribani 25,000 katika halmashauri za wilaya za Muleba, Ngara na Bukoba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara imesambaza seti 58 za vifaa vya umwagiliaji katika Halmashauri za Bukoba - 15, Ngara - 18, Muleba - 10 na Missenyi 15 na kuanzisha vituo vitatu vya kutoa zana za kilimo katika Halmashauri za Missenyi, Muleba na Karagwe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Neema Majule, swali la nyongeza.

MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri yanayoonyesha kweli Serikali imefanya jitihada kubwa kuhakikisha wakulima hawa wanapata nafuu na pia wanapata huu ujuzi na hata kuweza kujengewa uwezo.

Je, Serikali ina mpango gani sasa kuhakikisha kwamba wakulima hawa na hasa *exporters* wanapata nafuu ya bei kwa maana soko la kahawa linayumbishwa sana na bei ya soko la dunia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri kipindi kilichopita/awamu iliyopita/miaka mitano iliyopita Serikali yetu ilibainisha mazao ya biashara Tanzania nzima na kuyajengea uwezo yaani kuwajengea wakulima uwezo, na kama sisi hapa Dodoma zao letu sisi zabibu tunaita dhahabu ya Dodoma.

Swali langu ni hili hapa, Serikali imewekeza kiasi gani kwenye kutafiti na kutathmini mazao yetu yanapata nafasi kwenye soko la dunia hasa kuhimili ushindani wa bei? Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Majule kwa maswali mazuri ya msingi ambayo ameuliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ilikuwa ni kuhusu bei ya kahawa ambayo imekuwa ikiyumba kutokana na mabadiliko katika soko la dunia na mpango wa Wizara kwa maana ya Serikali katika kukabiliana na mabadiliko ya bei ilikuwa ni pamoja na kuanzisha Mfuko wa Kilimo kwa maana ya *(Agriculture Development Fund - ADF),* lengo lake tu ni kusaidia pale ambapo kunakuwa na mabadiliko ya bei ili kumsaidia mkulima kumkwamua katika kipindi cha kiwango cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hiyo ni sehemu ya mpango ambao tuko nao na ndiyo jitihada kubwa ambayo tumekuwa kukiifanya, lakini katika wakati mwingine tunaoendelea kufanya ni kuhimiza sasa matumizi ya kahawa ndani ya nchi, lakini na kuongeza *value* ya ile kahawa badala ya kuiuza ikiwa *raw* kwa maana ya malighafi, iuzwe ikiwa imeshakuwa *semifinished* au *finished product* kwenda kwa ajili ya mauzo zaidi. Kwa hiyo hizo ndiyo hatua ambazo sisi Serikali tumekuwa tukizifanya kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwekezaji, tumefanya uwekezaji mkubwa wa kuhakikisha kwamba tunapata bei nzuri kwenye masoko yote hapa nchini na ndiyo maana katika maelekezo ambayo tunayafanya sasa hivi, ni pamoja na kutumia Balozi zetu nje ya nchi kutafuta masoko kwa ajili ya bidhaa zetu ikiwemo zao la zabibu ambalo linalimwa hapa nchini.

Kwa hiyo, tunaendelea kufanya hivyo na tutaendelea kuwekeza fedha nyingi ili mazao yetu yaweze kupata bei nzuri na ya uhakika kwa ajili ya faida ya wakulima na nchi yetu kwa ujumla. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rebeca Nsemwa, swali la nyongeza.

MHE. REBECA S. NSEMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Njombe ni mkoa ambao umebarikiwa kuwa na matunda mengi ya aina mbalimbali ambayo hayapatikani maeneo mengi, lakini matunda hayo yamekuwa hayawanufaishi wananchi kwani hayana mpango wowote wa kuweza kununuliwa.

Je, ni lini Serikali itaweka kiwanda cha kusindika matunda katika Mkoa wa Njombe ili Wananchi wa Mkoa wa Njombe waweze kunufaika na mazao hayo?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninampongeza dada yangu Mheshimiwa Rebeca Nsemwa, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ninamuhakikishia, Mpango wa Serikali na ninasema vilevile mpango wa Waziri wangu wa sasa, Mheshimiwa Chongolo, moja ya mazao anayoyahimiza sana ni pamoja na kilimo cha *apple* ambacho kinafanyika sana Mikoa ya Iringa na Njombe, lakini vilevile tumeanza na hapa

Dodoma. Kwa hiyo, utaona kwamba jitahada yake kubwa ni kuhakikisha kwamba kilimo cha matunda kinaleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mipango aliyotuelekeza pale Wizarani, ni kwamba sasa kwa kutumia ule Mfuko wetu wa *ADF*, tutaanza kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya kuongeza thamani na yeye kwa sababu anatokea huko huko Njombe, basi moja ya maeneo ambayo tutayapa kipaumbele ni mkoa huo, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kenneth Nollo, swali la nyongeza.

MHE. KENNETH E. NOLLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu kwa kiasi kikubwa bado wakulima wanatumia jembe la mkono katika kilimo na kwa kuwa hawawezi wakaenda kutoka kwenye jembe la mkono wakarukia kwenye matumizi ya matrekta, yapo majembe ya ng'ombe.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa kwanza kodi zote kwenye jembe linalokokotwa na ng'ombe ili wakulima sasa waanze kuhamasika kutumia majembe yanayokokotwa na ng'ombe kuachana na jembe la mkono? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninamshukuru Mheshimiwa Kenneth Nollo, Mbunge wa Bahi kwa swali la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge anafahamu jitihada kubwa ambayo Serikali imeifanya katika kupunguza kodi kwenge zana za kilimo ikiwemo matrekta, *power tillers*, mashine za kupulizia, lakini vilevile pamoja na majembe. Kwa hapa nchini, vitu ambavyo vina msamaha wa kodi ni pamoja na vifaa vingi ambavyo vinaletwa kwenye sekta ya kilimo. Kwa hiyo Serikali itaendelea kulizingatia hilo na kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa sasa wa Serikali ni kujenga vituo vya zana za kilimo *(mechanization centres)* katika halmashauri zote nchini ili wakulima waweze kupata huduma za kulimiwa kwa gharama nafuu na ziweze kuwafikia wote hapa nchini. Huo ndiyo mpango ambao tuko nao na mpaka sasa hivi tumeshafungua vituo 79 kati ya 1,000 ambavyo tumepanga kuvifungua. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla hatujaenda kutafuta masoko ya nje, kumbuka kuna masoko ya ndani ambapo kumekuwa na changamoto ya wafanyabiashara kwenda moja kwa moja kwenye mashamba ya wakulima na kununua mazao, tena wafanyabiashara kutoka nje ya nchi tofauti na nchi nyingine ambavyo wanafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni upi mkakati wa Serikali hususan kwa Wilaya ya Makete na Mkoa wa Njombe ambapo wakulima wamekuwa wakikutana na wafanyabiashara kutoka nje moja kwa moja na wamekuwa wakinyonywa kiasi kwamba kilimo hakijawa tena chenye tija kwao kama ambavyo Serikali imekuwa ikihimiza?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninampongeza vilevile Mheshimiwa Mbunge wa Makete, kaka yangu Mheshimiwa Festo Sanga na ninamthibitishia tu kwamba kwenye soko la ndani mpango mkakati wa Serikali wa sasa, moja tunataka kujenga masoko ambayo biashara zote za mazao hapa nchini kwenye kila halmashauri zitakuwa zinafanyika na hapatakuwa na watu ambao watakuwa wanakwenda mashambani kwa ajili ya kuwanyonya wakulima moja kwa moja. Kwa hiyo, lazima tutengeneze eneo tunasema *aggregation centre* ambayo itawakutanisha wakulima na wafanyabiashara, ndiyo jukumu kubwa ambalo sisi Serikali sasa hivi tunalifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maelekezo ya Serikali kupitia Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi kule chini kuhakikisha kwamba wanazuia hiyo hulka ya watu kwenda mashambani kuwanyonya wakulima kabla ya kumaliza kile kipindi chao cha msimu wa kilimo na kuleta katika maeneo rasmi.

Kwa hiyo, ni mpango wa Serikali na sisi tunaendelea kulifuatilia, lakini tutaendelea kusukuma zaidi kujenga maeneo ambayo tutamkutanisha mkulima na mfanyabiashara kwa wakati mmoja, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa David Silinde, Naibu Waziri wa KIlimo, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, sasa ninamwita Mheshimiwa Dickson Nathan Lutevele, Mbunge wa Mafinga Mjini, aweze kuuliza swali lake.

Na. 550

Kutambuliwa kwa Mwanamke Kama Mrithi Halali wa Mali za Familia

MHE. DICKSON N. LUTEVELE aliuliza: -

Je, lini sheria itamtambua mwanamke kuwa mrithi halali wa mali za familia sawa na mwanaume?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Zainab Katimba.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya mirathi Tanzania yanaongozwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ambayo inatambua usawa baina ya wanaume na wanawake, Sheria ya Uthibitishaji wa Wosia na Mirathi Sura ya 352, Sheria za Kidini, Sheria za Kimila na Sheria ya Urithi ya India ya

mwaka 1865. Sheria zote hizo zimeainisha watu wanaotakiwa kurithi ni pamoja na wazazi, wenza kwa maana ya mke au mume na watoto. Hivyo, kwa mujibu wa sheria hizo, mwanamke anatambulika rasmi kuwa mrithi halali wa mali akiwa mama, mke au mtoto.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dickson Lutevele, swali la nyongeza.

MHE. DICKSON N. LUTEVELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro mingi ya mirathi nchini Tanzania inasababishwa sana na ndugu wa mume kudai mirathi huku wakidai kuwa mwanamke ni mrithi tu na siyo mmiliki halali wa mali jambo linalowapata wajane wengi sana hapa nchini. *(Makofi)*

Sasa je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuleta muswada Bungeni ili kuleta sheria itakayomtambua mwanamke kama mmiliki halali hasa ukizingatia kwamba kwa sasa wanawake wanashiriki sana katika shughuli za uzalishaji badala ya kumwacha mwanamke kusubiri kama warithi wengine pindi mumewe anapofariki? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuanza kwanza kumpongeza Mheshimiwa Dickson Nathan Lutevele kwa swali lake hili zuri kabisa ambalo linalenga kuleta usawa wa kijinsia kwa maana ya wanawake na wanaume, lakini pia ninaomba Umoja wa Wabunge Wanawake *(TWPG)* uweze kumtambua Mheshimiwa Dickson kama *champion* wa usawa wa kijinsia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye swali lake la kwanza la nyongeza, ninaomba kumjibu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye majibu ya msingi kwamba nchi yetu inaongozwa na misingi ya sheria na masuala ya mirathi pamoja na kwamba yanafuata sheria nyingine, lakini yanafuata misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ibara ya 12 na Ibara ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inazungumzia masuala ya usawa, usawa wa kijinsia na inakataza kabisa, ni tamko la Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inakataza ubaguzi kwa minajili ya kijinsia, kwa maana wanawake, watu wote ni sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa Sheria Mama ya nchi ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tafsiri yake ni kwamba hamna sheria nyingine yoyote ambayo inaweza kuwa na mazingira baguzi ya kijinsia.

Kwa hiyo, ninaomba kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba hata Mahakama pale inapotafsiri sheria mbalimbali katika mashauri mbalimbali, na ninatolea mfano kwenye kesi ya Ephraim dhidi ya Pastory, Mahakama ilieleza kwenye masuala ya mirathi kwamba mwanamke hatobaguliwa na ana haki sawa ya kurithi kama mwanaume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa kuangalia jinsi gani sheria zetu za nchi kama Katiba zinavyosema, tukiangalia Mahakama inavyotafsiri sheria, ni dhahiri kwamba mwanamke ana haki sawa ya kurithi mali katika nchi hii ya Tanzania na ninaomba kutoa rai kwa Watanzania wote wanaonisikiliza kwa wakati huu, ninaomba tutoe elimu kwa wanawake waweze kuzifahamu haki zao za kimsingi ikiwemo haki katika mirathi/haki za kurithi ili wafahamu kwamba nchi yao hii ya Tanzania inawahakikishia na wenyewe wana haki sawa ya kurithi mali kama vile wanavyorithi wanaume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wakati huu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan tunatarajia siku ya tarehe 20 Juni, ataenda kuzindua Mradi wa *Mama Samia Legal Aid Campaign* awamu ya pili ambapo tunatoa huduma ya msaada wa kisheria kwa Watanzania. Ninaomba mjitokeze wale wote ambao mna changamoto za kisheria, wanawake ambao mna changamoto

ikiwemo changamoto katika masuala ya mirathi ili tuweze kuwahudumia. Watakuwepo wanasheria wa kutosha na nchi yenu na Serikali hii ya Awamu ya Sita inasimamia katika kuhakikisha wanawake mnapata haki zenu. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Janeth Mahawanga, swali la nyongeza.

MHE. JANETH E. MAHAWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi.

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha wanawake wanapata uelewa wa kutosha hususan kundi la wajane na mabinti kutokana na kukosa haki zao za msingi za urithi kwa sababu ya mila na desturi ambazo zinatoa unyanyasaji? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Janeth Mahawanga kwa swali lake hili zuri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali inafanya kazi kubwa sana ya kuelimisha umma na ninaomba tuungane pamoja ikiwemo nanyi Waheshimiwa Wabunge kuwaelimisha Watanzania kuhusiana na haki mbalimbali ikiwemo haki za wanawake ikiwemo kwenye masuala ya mirathi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukiacha na jitihada hizo, Sheria ya *JALA*, Sheria ya Mahakama na Matumizi ya Sheria *(Judicature and Application of Laws Act)* inatambua kwamba kuna Sheria za Kimila. Sheria za Kimila zinatambulika na Watanzania wanaweza kuzitumia, lakini sheria hizi zinatumika zile ambazo tu hazikinzani na sheria nyingine zilizotungwa na Bunge, hazikinzani na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hazikinzani na haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba kutumia fursa hii kuendelea kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge Janeth

Mahawanga kwamba Serikali itaendelea kuelimisha Watanzania ikiwemo wanawake na mabinti wafahamu haki zao za kimsingi ili wafahamu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasimamia katika usawa ambao umewekwa katika misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 12 na Ibara ya 13. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Stella Ikupa, swali la nyongeza.

MHE. STELLA I. ALEX: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kuwa kumekuwa na changamoto kubwa ya watu kuondoka duniani ama kufariki bila kuacha wosia, na hii inapelekea changamoto kwa wanaobaki. Nini mkakati wa Serikali kutoa elimu kwa Watanzania kuhusu masuala ya wosia?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake hili zuri sana na ninaomba kutumia fursa hii kuwaomba Watanzania, lakini kuwaomba Waheshimiwa Wabunge muungane na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuwahamasisha Watanzania waweze kufahamu kwamba kuandika wosia ni jambo la muhimu sana. Mara nyingi watu hawapendi kuzungumzia masuala ya wosia na kumekuwa na mila na desturi ambazo zinawafanya Watanzania waone kama wosia siyo kitu cha kujadiliwa au kitu cha kufanya au kinaleta mikosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni utaratibu mzuri sana ambao unaweza ukafuatwa ambao unaweza ukasababisha kupunguza migogoro inayojitokeza pindi pale mtu anapokuwa ametangulia mbele ya haki bila kuwa ameacha wosia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kupitia *RITA*, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inafanya kazi hiyo ya kuhamasisha na kutoa elimu kwa Watanzania, lakini ninaomba Waheshimiwa Wabunge tuungane kwa pamoja ikiwemo ninyi wenyewe kuwa mfano katika kuandika wosia, lakini kuwahamasisha na Watanzania waweze kuandika wosia kwa maana ni utaratibu

mzuri ambao unaweza ukasaidia kupunguza migogoro inayohusiana na masuala ya mirathi. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zainab Katimba, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, sasa ninamwita Mheshimiwa Dkt. Yahya Esmail Nawanda, Mbunge wa Newala Vijijini aulize swali lake. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Rashid Mohamed Mtima.

Na. 551

Kuimarisha Chuo cha *VETA* Kitangali

MHE. RASHID M. MTIMA K.n.y. MHE. DKT. YAHYA E. NAWANDA aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha Chuo cha *VETA* kilichopo katika Mji wa Kitangali?

MWENYEKITI: Majibu, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Wanu Hafidh.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ninaomba kujibu swali namba 551 la Mheshimiwa Dkt. Yahya Esmail Nawanda, Mbunge wa Newala Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha *VETA* cha Wilaya ya Newala ni miongoni mwa vyuo 12 vya *VETA* vilivyopokelewa kutoka halmashauri na wadau mbalimbali ambavyo vinaendelea kuboreshwa kupitia fedha za mapato ya ndani ya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi *(VETA)* ili viweze kufikia viwango vya chini vinavyotakiwa *(minimum verifiable standards)* kwa vyuo vya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Serikali ilipokabidhiwa Chuo cha *VETA* cha Wilaya ya Newala, imefanya ukarabati mkubwa wa majengo yaliyokuwa chakavu pamoja na ujenzi wa majengo mapya ikiwemo jengo la utawala, karakana, madarasa, mabweni na nyumba ya Mkuu wa Chuo. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imeshatumia kiasi cha shilingi milioni 66.3 kati ya shilingi milioni 100 zilizokuwa zimetengwa. Aidha, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali imetenga shilingi milioni 81.1 kwa ajili ya ukarabati na uboreshaji wa bwalo na jiko. Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu mingine kwa kadri ya uwezo wa fedha utavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rashid Mtima, swali la nyongeza.

MHE. RASHID M. MTIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninachukua nafasi ya kuishukuru Serikali kwa jitihada zinazoendelea kuimarisha Chuo cha Ufundi pale *VETA* Kitangali. Pamoja na jitihada hizo, ninaomba kuuliza maswali mawili yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Chuo cha Ufundi Kitangali kuna uhaba mkubwa sana wa wakufunzi katika fani mbalimbali. Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba pale wanapeleka wakufunzi wa fani zile ili wananchi wa Newala na maeneo mengine waweze kufundishwa masuala ya ufundi yanayotolewa katika chuo kile?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kama majibu ya Serikali yanavyosema kwa sasa ni nyumba ya Mkuu wa Chuo tu imejengwa pale, lakini tunatambua Kitangali ni Mji mdogo na sasa Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Newala yapo pale, mahitaji ya makazi ni makubwa, je, Serikali ina mpango gani au ni lini Serikali itajenga nyumba za walimu na watumishi wengine pale Chuo cha Ufundi Kitangali ili kuondoa adha ya kuangaika na upangaji kule mtaani? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rashid kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Kitangali – Newala kina jumla ya walimu sita hivi sasa na mahitaji ya wakufunzi wa chuo kile kutokana na kozi zinazotolewa pale ni jumla ya walimu saba. Kwa hivyo, chuo kile kina upungufu wa mwalimu mmoja tu kwa ajili ya mafunzo haya ambayo ameyataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tayari kibali cha kuajiri walimu 700 kimetoka mwaka huu wa fedha 2025/2026 na hadi sasa ajira 200 zimeishajazwa na ajira 500 zipo katika hatua za kutangazwa.

Kwa hiyo, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kadiri tunavyoendelea kupokea waajiri wa mafunzo haya, basi tutaendelea kuwasambaza kwa vile vyuo ambavyo vina upungufu wa walimu hawa ikiwemo Chuo cha Kitangali, Newala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, Serikali ni kweli imekamilisha ujenzi wa nyumba moja ya mtumishi ambayo inatumiwa na Mkuu wa Chuo pale, lakini pia Serikali imekamilisha tathimini ya nyumba tatu ambazo zimechakaa na marekebisho ya nyumba zile ni makubwa, lakini tayari takribani shilingi milioni 124 zimeshatengwa kwa ajili ya marekebisho haya na *once* marekebisho haya yatakapokamilika basi watumishi na walimu wa Chuo cha Kitangali pale Newala watatumia nyumba hizi kwa ajili ya huduma.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Rashid kwamba tunaenda kukamilisha marekebisho ya nyumba zile tatu zilizochakaa na zitatumika kwa ajili ya watumishi wa chuo kile cha Kitangali. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Wanu Hafidhi, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa tunaendelea sasa ni Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, namwita Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrew, Mbunge wa Viti Maalum aweze kuuliza swali lake. *(Makofi)*

Na. 552

Uwekezaji wa Pesa kwa Jeshi la Zimamoto – Wilaya ya Urambo

MHE. MHE. JUMA M. KAWAMBA K.n.y. MHE. JACQUELINE K. ANDREW aliuliza:-

Je, lini Serikali itawekeza fedha kwenye Jeshi la Zimamoto Wilayani Urambo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, Mambo ya Ndani, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrew, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na jitihada za kuwekeza fedha katika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji nchini kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za maokozi katika maeneo yao kwa wakati ambapo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imewekeza jumla ya shilingi 18,013,513,000 na kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Bunge lako Tukufu liliidhinisha jumla ya shilingi 28,013,513,000 sawa na ongezeko la 55.5% ya bajeti iliyopita. Katika mwaka wa fedha 2027/2028 Serikali kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linatarajia kujenga Kituo cha Zimamoto na Uokoaji katika Wilaya ya Urambo, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kawamba Mustafa, swali la nyongeza.

MHE. JUMA M. KAWAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza napenda kuishukuru Serikali kwa kazi nzuri inazoendelea kufanya kupitia hii Wizara ya Mambo ya Ndani.

Swali la kwanza, Serikali haioni haja ya kuongeza msawazo wa ikama ya watumishi wa Jeshi la Uokoaji na Zimamoto kwani watumishi waliopo sasa ni wachache hawakidhi changamoto za kiwilaya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali namba mbili Serikali ina mpango gani juu ya uwepo wa vifaa vya uokoaji na zimamoto hususan magari ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Uyui hasa kwenye Jimbo la Igalula? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nishukuru sana kwa maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kawamba ambapo swali la kwanza lilieleza kwamba je, Serikali haioni haja ya kuongeza ikama ya watumishi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaona haja ya kuongeza ikama ya watumishi kila mahali au kila wakati uhitaji unapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wakati huu tunapozungumza, naomba nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba wapo vijana wetu ambao wapo kwenye mafunzo na muda siyo mrefu watamaliza mafunzo, wakimaliza mafunzo wataweza kugawanywa kwenye maeneo mbalimbali likiwepo eneo lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa eneo la vifaa, naomba tu niseme kwa ujumla kwamba kwa ukweli Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hasa katika eneo hili ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji imeweka historia katika Taifa hili na moja ya historia hiyo ni kwamba hali ya huduma za zimamoto na uokoaji nchini hadi

mwaka 2024 zilikuwa zipo katika asilimia tano lakini mwaka huu wa 2026 hali ya utoaji wa huduma za zimamoto na uokoaji zipo katika 80% hilo ni ongezeko kubwa mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba vifaa vya zimamoto na uokoaji vinaendelea kusambazwa kama ambavyo tumetoa taarifa ya awali wakati tukijibu maswali katika maeneo mbalimbali nchini. Katika usambazaji huo kwa sasa wilaya 102 zina vifaa kwa ukamilifu, na ni wilaya sita tu ndiyo hazijafikiwa kabisa na huduma za zimamoto na uokoaji. Tunaamini kwamba kwa uwekezaji huu nilioutaja na ule ambao utawekezwa zaidi basi hali ya utoaji wa huduma itaimarika zaidi, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ayoub Mohammed, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, sasa namwita Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Kinondoni, aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 553

Kuzipa Manispaa za Mkoa wa Dar es Salaam Mamlaka ya Kushughulikia Masuala ya Ardhi

MHE. TARIMBA G. ABBAS aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kuzipa Manispaa za Mkoa wa Dar es Salaam mamlaka ya kushughulikia masuala ya ardhi ikiwemo utoaji wa hati za umiliki?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Kinondoni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa ardhi nchini umewekewa utaratibu mzuri katika Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 (Toleo la mwaka 2023) pamoja na Sheria ya Ardhi Sura ya 113 na 114. Kwa mujibu wa sera na sheria hizo, ardhi yote ni ya umma na imekabidhiwa kwa Mheshimiwa Rais kama mdhamini kwa niaba ya raia wote. Majukumu haya Mheshimiwa Rais ameyakasimu kwa Kamishna wa Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ikiwa ni msimamizi wa masuala ya ardhi kisera, ina watendaji kuanzia ngazi ya Taifa hadi Halmashauri. Watendaji hawa wamekasimiwa majukumu ya kiutendaji, hivyo masuala ya ardhi yamekuwa yakishughulikiwa hata katika ngazi za halmashauri ikiwemo utayarishaji wa hati za umiliki wa ardhi. Aidha, ieleweke kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Mipangomiji, Sura ya 355, halmashauri zimetambuliwa kuwa Mamlaka za Upangaji, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tarimba Abbas, swali la nyongeza.

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, namshukuru pia Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba Jiji la Dar es Salaam linakuwa kwa kasi sana na lina sadikiwa kuwa ni Jiji la tatu kwa ukuaji wa zaidi ya asilimia nane kwa mwaka nyuma ya Lagos na Addis Ababa.

Mheshhimiwa Mwenyekiti, shughuli za Dar es Salaam katika masuala ya kushughulikia changamoto za ardhi zimekuwa ni nyingi; je, Serikali haioni sababu badala ya kuwa na Makamishna Wasaidizi kwenye ngazi ya mkoa wakafanya Makamishna Wasaidizi wawe katika ngazi ya wilaya ili kuharakisha shughuli za

uhitaji wa ardhi ziende kwa kasi kama Jiji linavyokua? Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba Dar es Salaam inaondoka katika mji ambao unachelewa kupangwa kuwa ni mji wenye kupangwa ili kuondokana na ujenzi holela na hasa *squatters* ambazo zinaenea kwa kila mahala? Nakushukuru sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge wa Kinondoni Ndugu Tarimba Gulam Abbas, amekuwa mstari wa mbele siku zote kupambania mabadiliko ya Mkoa wa Dar es Salaam na hususan kwenye eneo hilo la upimaji, upangaji na umilikishwaji wa maeneo katika mkoa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Mkoa wa Dar es Salaam ni Mkoa ambao unakua kwa kasi sana na una watu wengi sana na shughuli hizi za watu kuhitaji kupimiwa maeneo, kupangiwa maeneo na kumilikishwa ni nyingi sana katika huu Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuliona hili Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanya mapitio ya muundo wa usimamiaji wa shughuli za masuala ya ardhi katika huu Mkoa wa Dar es Salaam. Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan mnamo tarehe 4 Machi amesaini muundo mpya katika mikoa mitatu kama ifuatavyo ili kuhakikisha kwamba huduma hizi za masuala ya ardhi zinawafikia wananchi vizuri:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mkoa wa Dar es Salaam, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ameanzisha Ofisi ya Ardhi ya Mkoa wa Dar es Salaam kanda namba moja ambayo itakuwa

na Wilaya ya Ilala, Temeke pamoja na Kigamboni ili kusogeza huduma karibu kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu Mheshimiwa Rais pia ameanzisha Ofisi ya Ardhi, Mkoa wa Dar es Salaam kanda namba mbili ambayo itajumuisha Kinondoni na Ubungo. Hivyo hivyo, kwa Mkoa wa Mwanza kwa sababu nao una sura kama ilivyo Dar es Salaam, Mheshimiwa Rais kupitia huu Mkoa wa Mwanza anakwenda kuanzisha Ofisi ya Ardhi ya Mkoa wa Mwanza kanda namba moja ambayo itajumuisha Wilaya za Ilemela na Nyamagana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kutakuwepo na Ofisi ya Mkoa ya Ardhi ya Mwanza kanda namba mbili ambayo yenyewe itabeba Wilaya za Sengerema, Magu, Kwimba, Misungwi pamoja na Ukerewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo, Mheshimiwa Rais kwa kutambua umuhimu na ukuaji wa Jiji la Dodoma ameanzisha Ofisi ya Ardhi, Mkoa wa Dodoma kanda namba moja ambayo itahusisha Dodoma Mjini pamoja na Chamwino.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tutakuwa na Ofisi ya Ardhi, Mkoa wa Dodoma kanda namba mbili itakayohusisha Wilaya za Kondoa, Bahi, Chemba, Kongwa pamoja na Mpwapwa, lakini vilevile kama mnavyofahamu miaka hii ambayo Mheshimiwa Rais amekuwepo madarakani amekuwa ni *champion* namba moja katika kuvutia wawekezaji wa ndani na wa nje, hivyo ameamua pia kuanzisha Ofisi ya Ardhi na kuanzisha Mkoa Maalum wa Kiuwekezaji ndani ya *TISEZA* kwa maana ya Mamlaka ya Uwekezaji pamoja na maeneo ya kiuchumi nayo itakuwa na mkoa maalum wa ardhi ambao kama ilivyo mikoa mingine hii iliyoanzishwa itakuwa inasimamiwa na Makamishna Wasaidizi. Muundo huu utaanza kutumika mapema mnamo mwaka wa fedha huu tunaokwenda kuuanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali la pili Mheshimiwa Mbunge ametaka kufahamu mpango wa kuhakikisha Dar es Salaam haiendelei kuwa na makazi holela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwenye Mkoa wa Dar es Salaam tunao mpango wa miaka 10 ambao tumeanza kuutekeleza kuanzia mwaka 2016 na tutakwenda nao mpaka 2046.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mpango huu tumeanza kwa kuhakikisha tuna rasimisha makazi yote ambayo yalijengwa bila kupimwa ambayo yana sifa kisheria, tuna rasimisha kuyapima na kuyamilikisha wananchi kihalali, lakini vilevile maeneo ambayo yapo pembezoni mwa miji tunatangulia kwenda kuyapima ili watu watakapofika kwenye maeneo hayo kusiwe na uholela wa makazi kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, kwa maeneo ambayo yalijengwa zamani bila kuzingatia upimaji tunao mpango unaoitwa *land re-adjustment* ambao tunafanya mapitio ya maeneo hayo na kuyajenga upya ama kwa sisi wenyewe Serikali au kwa kushirikisha sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo, siku za karibuni tumeweka mpango mkakati maalumu kabisa kwa ajili ya kuongeza udhibiti katika ujenzi kwa kuhakikisha ujenzi wote ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam unafanyika kwa kuzingatia sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho tunawashirikisha sekta binafsi katika upimaji, uthamini pamoja na umilikishaji wa ardhi ili kuhakikisha tunatanua wigo mpana, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kwagilwa Reuben, Naibu Waziri Muungano na Mazingira tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu, naomba nianze kwa kuwatambulisha wageni walioko Bungeni asubuhi ya leo.

Wageni 67 wa Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini ni wanafunzi na walimu wa Shule ya Msingi Nalopa kutoka Jijini Arusha. *(Makofi)*

Wapo pia wageni 61 wa Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro ambao ni wanafunzi na walimu wa Shule ya *St. Joseph* kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni 28 wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe ambao ni Kwaya ya *Prospect Singers* kutoka Kanisa la Waadventista Wasabato Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wengine wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni Maaskofu, Wachungaji, Wanamaombi, Mwalimu wa Neno la Mungu na timu yake yote kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; ni wanafunzi 99 na walimu nane wa Shule ya *St. Mary's International* kutoka Mkoani Morogoro. *(Makofi)*

Wapo pia wanafunzi na walimu wa Shule ya *St. Joseph The Worker* kutoka Kibada Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni wetu wote karibuni hapa Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba nilete kwenu tangazo; tangazo la kwanza linatoka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club,* Mheshimiwa Rebeca Nsemwa anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge na watumishi wanamichezo kuwa kutakuwa kuna mechi ya kujipima nguvu kati ya Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Ofisi ya Bunge kwa michezo ya mpira wa kikapu *(basketball)* na kuvuta kamba kwa wanawake na ratiba ya michezo hiyo itakuwa kama ifuatavyo:-

Mpira wa kikapu kesho tarehe 10 Juni, 2026 *Chinangali Park* saa 12.00 asubuhi; na pia kuvuta kamba siku ya Alhamisi tarehe 11 Juni, 2026 Uwanja wa Jamhuri saa 12.00 asubuhi. Mnaombwa wote kujitokeza kwa wingi kuziona timu zetu za Bunge

zinazoendelea na maandalizi ya Michezo ya Mabunge ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Pia, lipo tangazo linatoka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club,* anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba leo tarehe 9 Juni, 2026 mara baada ya Kikao cha Bunge kutakuwa na kikao cha viongozi wa *Bunge Sports Club*. Kikao hicho kitahudhuriwa na Wajumbe wa Kamati ya Utendaji pamoja na Manahodha wote wa Michezo ya *Bunge Sports Club* katika ukumbi namba 9 uliopo Jengo la Utawala, *ground floor* hivyo, Wajumbe wote mnaombwa kufika kwa wakati bila kukosa. *(Makofi)*

Pia, lipo tangazo linatoka kwa Katibu wa Bunge, Waheshimiwa Wabunge wote mnataarifiwa kuwa leo mara baada ya kuahirishwa kwa Shughuli za Bunge yatafanyika mafunzo mafupi ya utayari wa majanga ya moto, mafunzo haya yatafanyika humu ndani ya ukumbi wa Bunge. Hivyo, Waheshimiwa Wabunge tunaombwa na kusisitizwa mara baada ya kuahirisha Bunge tubaki humu ndani ili kufahamu jinsi ya kujiokoa na majanga ya moto. *(Makofi)*

Imetolewa na Katibu wa Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema haya naomba kuahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

(Saa 5.19 Asubuhi Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 10 Juni, 2026 Saa Tatu Asubuhi)

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA
UHURU
na
UMOJA